# Nipashe

Jumatatu Aprili 27, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580216

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

...rdian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




TOLEO MAALUMU

## Misa Tan: Dk. Mengi alitufanya kuwa sauti moja yenye nguvu

UKURASA 3




UKURASA 11

# Sukari tani 23 yanaswa ikiuzwa kwa ulanguzi

• **Ilifichwa** kwenye maghala, wafanyabiashara wakubwa wamo, ya kutoka nje ya nchi nayo mbaroni... *Endelea ukurasa 2*



Maofisa wa Polisi kwa kushirikiana na maofisa kutoka Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), wakikagua shehena ya sukari kutoka nje iliyokamatwa kwa mmoja wa wafanyabiashara wakubwa katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## Mbaroni tuhuma za kunywesha mtoto bia

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Wizara kufuatilia shule 500 utekelezaji sheria

UKURASA 2



### BAA LA CORONA

**Kama umekuwa karibu na mtu mwenye Covid -19, uwezekano wa kuambukizwa ni mkubwa. Kuwa karibu ina maana uko na mtu huyo au umekaa naye ndani ya mita moja. Unapogundua hali hiyo ni vizuri ukajitenga kwa kukaa nyumbani.**

**WHO**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**


**MICHEZO** **SAMATTA AFYEKWA MSHAHARA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Waliomnywesha bia mtoto wa miaka 3 mbaroni

**Na Ndalike Sonda,** SHINYANGA

WATU watatu wanashikiliwa na Polisi Mkoa wa Shinyanga kwa tuhuma za kumpeleka mtoto wa miaka mitatu baa na kumywesha bia huku wakimchukua video na kuisambaza kwenye mitandao ya kijamii.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga ACP, Debora Maligilimba, ilisema watuhumiwa hao walitenda kosa hilo, Aprili 24, majira ya saa sita mchana, katika baa moja Kijiji cha Nyaligongo, Kata ya Mwakitolyo.

Kamanda Magiligimba alisema, kitendo hicho ni ukatili dhidi ya mtoto na matumizi mabaya ya kimtandao na kwamba waliomnywesha bia walisikika wakimwambia amalize wampe nyingine.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Godius Katisha (32), mkazi wa Mwakitolyo ambaye ni mmiliki wa baa hiyo, Alphonce Pima (32), mkazi wa Mwakitolyo na Oscar Makondo (35), mkazi wa Mtaa wa Mayila Mjini Kahama.

Kamanda Magiligimba alisema baada ya tukio hilo kuonekana kwenye mitandao ya kijamii, kikosi kazi cha askari wa uhalifu wa makosa ya kimtandao waliwakamata watuhumiwa hao akiwamo Katisha ambaye ni baba mzazi wa mtoto huyo. Watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Kamanda Magiligimba aliwataka wananchi kuheshimu haki za mtoto na yeyote atakayeenda kinyume hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Juzi baada ya video hiyo kusambaa kwenye makundi ya mtandao wa Whatsapp, wananchi waliomba hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa wahusika ikiwamo kuwafikisha mahakamani pamoja na kuifunga baa hiyo.



Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania PLC, Hisham Hendi, akimkabidhi zawadi ya simu mteja wa Vodacom, Abutwalib Mtua, alipotembelea duka la kampuni hiyo makao makuu kuangalia namna watoa huduma wanavyowalinda wateja wao kipindi hiki cha corona kwa kusisitiza uvaaji wa barakoa, kuwapima joto na kuwapa vitakasa mikono waingiapo kupata huduma kwenye maduka ya kampuni hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# Sukari tani 23 yanaswa ikiuzwa bei ya ulanguzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BODI ya Sukari Tanzania (SBT), imekamata shehena ya sukari zaidi ya tani 23.

Kiasi hichi kinahusisha sukari iliyoagizwa nje ya nchi na ya ndani, ikiuzwa kwa bei ya ulanguzi, tofauti na bei elekezi iliyotangazwa na serikali wiki iliyopita.

Walionaswa na sukari hiyo walikuwa wameificha kwenye baadhi ya maghala, wakiwamo wafanyabiashara wakubwa katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Katika operesheni hiyo maalum iliyoendeshwa jana kwa usiri na maofisa wa bodi hiyo wakishirikiana na askari kanzu wa Jeshi la Polisi, Nipashe ilishuhudia sukari hiyo ikizuiwa isiendelee kutumika hadi hapo serikali itakapotoa maelekezo mengine.

Ofisa Mwandamizi wa Udhibiti wa SBT, Faustine Mgimba, akizungumza baada ya operesheni hiyo, alisema wamebaini sukari hiyo ilikuwa ikiuzwa kwa walaji kwa bei ya rejareja ya Sh. 3,400 tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,700 kwa kilogramu moja kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Tanga na Morogoro.

Wafanyabiashara hao, walitumia pia ujanja wa kuuza mfuko mmoja wa sukari wa kilogramu 50 kwa Sh. 135,000 ambayo ni tofauti na bei elekezi ya Sh. 128,000.

Zaidi Mgimba alieleza: "Tumegundua kwamba changamoto kubwa katika maduka mengi, wafanyabiashara wameshindwa kuwa wa kweli, wengi wao hawajaweza kuonyesha nyaraka za uagizaji sukari kutoka kwa mawakala wakubwa ili kuthibitisha uagizwaji wake.

"Na baadhi yao wameficha kiasi kikubwa cha sukari ili kuuza kwa bei kubwa, kitu ambacho ni kuwakandamiza walaji." Katika operesheni hiyo, maofisa wa SBT pia walikamata gari dogo aina ya Pick Up iliyokuwa ikitorosha sukari hiyo ili kuepuka mkono wa dola.

Aprili 23, mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitangaza bei elekezi ya sukari kwa kila mkoa nchini, huku akiwaonya watakaobainika kuuza kinyume cha utaratibu huo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, ikiwamo kunyang'anywa leseni za biashara. Sheria ya Sukari Na. 26 ya Mwaka 2001 chini ya kifungu cha 11A, inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya kilimo, kutangaza bei ya ukomo wa juu ya sukari.

Waziri Hasunga alinukuliwa akisema bei hiyo elekezi imepangwa kwa kuzingatia gharama zote za uagizaji wa sukari ya kuziba pengo zinazotumiwa na wazalishaji kuagiza sukari kutoka nje ya nchi na umbali wa kila eneo.

Hata hivyo, baadhi ya maofisa mauzo na ugavi katika maduka makubwa yaliyonaswa na sukari hiyo, walidai wameagiza sukari kutoka jijini Dar es Salaam kwa wakala mmoja.

Wakati operesheni hiyo ikiendelea, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alikwenda katika Kiwanda cha Sukari cha TPC, ambapo alieleza kuwa serikali imeagiza tani 40,000 kwa ajili ya kuongeza usambazaji wa sukari sokoni mpaka pale viwanda vya ndani vitakapoanza uzalishaji.


**Enabel** Belgian Development Agency

**CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST**

**PROMOTION OF SANITATION AND HYGIENE IN KIGOMA**

The Kingdom of Belgium through Enabel and the Government of Tanzania through the Ministry of Water, are implementing a water and sanitation project in Kigoma region. This is a 5-year project which runs through June 2022 and aims to promote provision of sustainable water supply services in the region. The project now seeks to engage an NGO to carry out activities that aim at improving safe hygiene practices at household level in respective of: a) water collection, b) transport to point of use, c) storage d) use e) hand-washing and f) latrine use.

Interested NGOs can be local or international or a partnership of both but with a track record in carrying out sanitation and hygiene promotion activities using the most effective approaches. The project is looking for NGOs with capacity to implement and monitor and evaluate improvements in hygiene practices. Those organizations that are directly present or have implementing partners in Kigoma region will have an added advantage

More information and bid documents of this assignment are available at: **https://btctanzania.wordpress.com/**

215716201


# Wizara kufuatilia shule 500 utekelezaji sheria

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema itafanya ufuatiliaji na tathimini katika shule 500 kuangalia utekelezaji wa sheria na miundombinu.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, wakati akiwasilisha makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2020/21.

Alisema katika kutekeleza jukumu la kusimamia sera na kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo, serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 200 zilizopatiwa usajili ili kuhakiki uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za usajili wa shule.

Vile vile, itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 100 zilizosajiliwa kwa masharti, ili kuona kama zimekamilisha miundombinu iliyokuwa haijakamilika.

Pia, itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 200 ili kuhakiki kama walimu wa kigeni wanafundisha kwa mujibu wa leseni zao.

"Tunatarajia kuandaa mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini wa ujenzi na ukarabati wa shule ili kuwezesha wadau wote wa shule kufuatilia na kutathmini maendeleo ya ujenzi,"alisema na kuongeza:

"Pia, itakamilisha uandaaji wa mfumo wa kieletroniki wa usajili wa shule za awali na msingi, vyuo vya ualimu na vituo nje ya mfumo rasmi ili kuhakikisha usajili wa shule unafanyika kwa uwazi."

Waziri Ndalichako alisema katika kuboresha elimu msingi na sekondari, serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji na usimamizi wa vituo shikizi vya shule katika mikoa 15 ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kuchukua hatua stahiki.

Kadhalika, itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule za Ufundi, Kilimo na shule za Michezo, ili kutathmini hali ya miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa mujibu wa waziri huyo, serikali itatoa mafunzo ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shuleni kwa walimu 200 wa shule za sekondari, ili kuwajengea uwezo na kuimarisha stadi za utoaji wa huduma za malezi shuleni.

Pia, itasambaza mwongozo wa malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shuleni katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ili kuimarisha utoaji wa huduma za malezi shuleni.

Kwa upande wa elimu maalum, serikali itaendesha mafunzo kazini kwa walimu wenye taaluma ya elimu maalum 350 wa shule za msingi na 150 wa shule za sekondari. Alisema kwa upande wa lugha ya alama, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, na Tehama ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni, itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule za sekondari 26, msingi 52, vyuo vya kati vitatu na vyuo vikuu saba vinavyopokea wanafunzi wenye ulemavu kwa ajili ya kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Waziri Ndalichako alisema kwa upande wa vyuo serikali kupitia idara ya uthibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu itafanya tathmini ya jumla katika asasi 6,020 zikiwamo shule za msingi 4,700, sekondari 1,200 na vyuo vya ualimu 120 na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu.

TOLEO MAALUM



## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Nina imani kuwa mojawawapo ya siri ya mafanikio na afya njema ni kufanya kazi kama punda, kupumzika kama mfalme."

# Misa Tan: Alitufanya kuwa sauti moja yenye nguvu

**Na Ali Othman**

"HAKUNA tulichoanzisha kama Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (Misa-Tan), akaacha kutusaidia kwa fedha na nafasi yake." Ni maneno ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Misa-Tan, Rose Haji Mwalimu.

Kwake, Rose anaona vyombo vya habari vinakosa mwelekeo hasa kwenye umoja wa wamiliki na kuwa na sauti moja yenye nguvu.

Wakati huu wa janga la Corona, anasema Dk. Mengi angesimama kama mfanyabiashara, mdau wa habari kuhakikisha kuna mazingira mazuri kwa wanahabari, kama siyo kwa kutoa fedha, lakini pia kwa mawazo ya nini kifanyike katika kuimarisha usalama wa wafanyakazi wa sekta hiyo.

Misa-Tan ilishirikiana naye kwa karibu, mfano kwenye maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa vyombo vya Habari kila Mei 3, iliyoasisiwa na Azimio la Windhoek, lililoanzishwa na taasisi hiyo na alishirikiana kwa kutoa rasilimali, muda na mawazo katika kufanikisha maadhimisho hayo kila mwaka.



Dk. Reginald Mengi akizungumza na katika moja ya mikutano ya wanahabari. **NA MPIGAPICHA WETU**

Anasema huwezi kuongelea uhuru wa kujieleza, upatikanaji wa habari na stahiki za sekta hiyo Tanzania na Afrika kwa ujumla, bila kumtaja Dk. Mengi, kwa kuwa amchango wake ulikuwa mkubwa kuhakikisha inastawi na kuwa endelevu.

"Nikiwa Mkurugenzi wa Misa-Tan, ndiye mtu wa kwanza kufadhili siku ya Uhuru wa Habari na kila mwaka alikuwa anatoa fedha Misa-Tan, aliahidi katika maisha yake yote na alifanya miaka yote," anasema.

### HABARI ZA UCHUNGUZI

Rose anasema wakati wanaendesha mradi wa MCT Bonga, kuhusu ufuatiliaji wa masuala ya rushwa kwenye serikali za mitaa, walipohitimisha walifanya kikao na Dk. Mengi na katika baadhi ya mapendekezo Misa-Tan ilipendekezwa kuwapo jopo la wahariri wa habari za uchunguzi.

"Kwa kuwa jukwaa ndiyo likikuwa linaanza na halina uwezo, alilipa ofisi ndani ya ofisi yake ya The Guardian Ltd na kuliwezesha katika mahitaji madogo madogo ya kujiendesha."

### TUZO ZA UMAHIRI

Misa-Tan ilianzisha tuzo za umahiri wa uandishi wa habari zikiitwa Edward Moringe Sokoine, Dk. Mengi alikuwapo kwenye jopo la watoa tuzo kwa waandishi mahiri wa uchunguzi, na kila mwaka alichangia fedha ikiwamo kushiriki.

"Alikuwa miongoni mwa tuzo za Edward Sokoine za habari za uchunguzi, ambayo kwa sasa ndiyo inaendeshwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) ikiitwa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), na kila mwaka alitoa fedha hata zilivyoanza kufanywa na Baraza hilo aliendelea kufanya hivyo."

> Nikiwa Mkurugenzi wa Misa-Tan, ndiye mtu wa kwanza kufadhili siku ya Uhuru wa Habari na kila mwaka alikuwa anatoa fedha Misa-Tan, aliahidi katika maisha yake yote na alifanya miaka yote.

"MOAT iliyoanzishwa chini ya MISA-Tan, iliwakusanya wamiliki wa vyombo vyote vya habari kuzungumzia masuala mbalimbali yanayovikabili vyombo hivyo kama mishahara, mazingira mabaya na mikataba kwa waandishi wa habari, uandishi usio na kimaadili, na maazimio mojawapo ni kuanzisha umoja wa wamiliki ambao utawaweka pamoja wamiliki ili wakae na kutoa mawazo yatakayochangia kuendeleza tasnia ya habari kwa kuzitatua changamoto zilizopo kwenye sekta hiyo," anabainisha.

Kabla ya mkutano huo, Roe na mwandishi wa siku nyingi, Lawrence Kilimwiko, walifanya utafiti kuangalia mazingira ya ufanyaji kazi ya waandishi Tanzania na kuja na matokeo ambayo yaliwasilishwa katika mkutano huo na ikaonekana kuna umuhimu wa wamiliki kuwa na umoja wao na kujadili masuala hayo na namna ya kuboresha.

Hapo ndipo kulipoanzishwa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari (MOAT) na Dk. Mengi akiwa Mwenyekiti wa kwanza.

Kwa mujibu wa Rose, Dk. Mengi alikuwa karibu na Misa-Tan kuhakikisha inakuwa kinara wa kusimamia haki na uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Mwenyekiti wa sasa wa Misa-Tan, Salome Kitomari, anasema huwezi kuzungumzia ustawi au safari ya vyombo vya habari Tanzania bila kumtaja Dk. Mengi kwa kuwa alihakikisha inastawi kwa kuhabarisha habari zinazodai uwajibikaji kwa wote wenye mamlaka.

"Nikiwa mwanachama wa Misa-Tan mara kadhaa nilishiriki mikutano, makongamano ambayo Dk. Mengi alikuwapo, aliwaasa sana wanahabari kuipenda taaluma yao, kuitetea na kufichua mambo yanayodai uwajibikaji kwa kuwa wao ndiyo jicho la wanao onewa, wanaoumia na wanaotumia vibaya madaraka na fedha za umma," anasema.

"Leo hii zaidi ya asilimia 90 ya waandishi wamepita kwenye vyombo vya habari vya IPP Media, wengi wenye majina makubwa na mafanikio makubwa wakiwa ndani na nje ya nchi wamefanyakazi ITV, Radio One, East Afrika, magazeti yaliyo chini ya kampuni ya The Guardian Ltd," anasema Kitomari ambaye pia ni Mwandishi wa habari Mwandamizi wa gazeti la Nipashe, mali ya kampuni za Dk. Mengi.

"Nimefanyakazi IPP Media tangu mwaka 2004, na niliajiriwa mwaka 2006, kama siyo maono ya Dk. Mengi kuwa na vyombo vya habari vingi na vilivyo imara, basi wapo ambao wasingekuwa na ajira au wasingepata nafasi ya kufanyakazi na kupata uzoefu katika fani ya habari," anasema.

Kitomari ambaye mwaka jana alikuwa mshindi wa jumla wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), anasema tasnia ya habari ina jukumu kubwa la kuayaishi yote yaliyoyaanzisha Dk. Mengi kwa kuwa ndiyo njia pekee ya kuimarisha, kuendeleza na kukuza sekta ya habari kwa maendeleo endelevu.

"Haifai kuzikumbuka jitihada zake bila kuziweka kwenye vitendo, amefanya mengo ya kukumbukwa kuhakikisha tasnia ya habari inapata heshima yake na hadi sasa tuna Sheria ya huduma za habari ya mwaka 2016 ambayo inaitambua tasnia ya habari kama taaluma rasmi, kabla ya hapo kila aliyejua kusoma na kuandika alikuwa mwandishi wa habari, lakini kwa sasa ni taaluma lazima uisomee."

Anasema Dk. Mengi aliwapenda waandishi na aliwasaidia mmoja mmoja au kupitia vyuo mbalimbali kuwapa ajira katika vyombo vyake, huo ulikuwa upendo wa hali ya juu kwa kuwa wapo wamiliki wenye uwezo. lakini hawajafanya aliyoyafanya.

***Mwandishi wa makala haya ni Mwanachama wa Misa-Tan, ambaye amewahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Taasisi hiyo.***

# Mpango wa Azaki kusaidia makundi maalum corona

**Na Enock Charles**

ASASI za Kiraia nchini, zimekabidhi kwa Serikali mpango mkakati wenye thamani ya Sh. bilioni 3 wa kukabiliana na janga la corona. Aidha, zimeainisha makundi mbalimbali ya kijamii yakiwamo walemavu ,wazee na watoto ambayo yataguswa na mpango huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, Onesmo Ole Ngurumwa, alisema taasisi hizo za kiraia takribani 200 zimeamua kuja na mpango mkakati huo ili kusaidiana na Serikali katika mapambano dhidi ya janga la corona.

"Sisi kama asasi za kiraia hatuwezi tukakaa tukajifungia ndani na kuiacha Serikali ikapambana yenyewe wakati na sisi tunaweza kuchangia chochote katika mapambano haya," alisema Ngurumwa.

Ngurumwa alisema asasi hizo zimefanya uchambuzi wa kina kuhusu madhara ya virusi vya corona na namna vinavyoathiri utendaji kazi wa asasi za kiraia nchini na kutoa mapendekezo kwa Serikali na asasi za ndani za kiraia zinavyoweza kufanya kazi kwa pamoja kusaidia kutokomeza virusi hivyo na majanga mengine ya aina hiyo.

Mbali na kusaidia makundi maalum ya kijamii, mpango mkakati huo unakusudia kusaidia katika baadhi ya maeneo ikiwamo utoaji wa vifaa tiba na kutoa elimu kuhusiana na janga la corona kwa namna mbalimbali. Akipokea mpango mkakati huo juzi, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Faustine Ndugulile, alisema mchango wa wadau katika mapambano dhidi ya janga la corona ni ya muhimu hasa katika kipingi hiki ambacho ugonjwa huo ni janga la kidunia.

"Sisi kama Serikali tunaupokea mpango huu kutoka katika jukwa la wana Azaki na wameainisha maeneo mbalimbali katika nyaraka yao, ya jinsi gani wanaweza kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya corona, mapambano haya yanamuhitaji kila mtu," alisema Dk Ndugulile.

Akizungumzia kuhusu vifaa vya kujikinga dhidi ya corona kwa madaktari wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa, Dk Ndugulile alisema Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba vifaa vya kujikinga dhidi ya ugonjwa huo linapewa kipaumbele cha kwanza ili kuhakikisha kuwa madaktari hao wanakuwa salama. "Hatuwezi kukubali mtumishi wetu wa afya akatoa huduma kwa mgonjwa bila kuwa na vifaa vya kujikinga, niwatoe wasiwasi watumishi, kipaumbele chetu cha kwanza ni kuhakikisha tunawalinda," alisema Ndugulile. Kauli hiyo ya Dk. Ndugulile, imekuja wakati ambapo Chama cha Madaktari Tanzania kimetoa angalizo la kuhakikisha kuwa watumishi wa afya wanapatiwa vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa corona wakati wanapotoa huduma kwa wagonjwa.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, akikagua bidhaa za wajasiriamali wadogo zinazochakatwa na mashine zilizotengenezwa na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO). **MPIGAPICHA WETU**

# Jela maisha kwa kubaka mtoto

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKAZI wa Kata ya Wailes, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Selemani Hassani (29), amehukumiwa kifungo cha maisha gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka minane (jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Lindi, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Batraine alimuuliza mshtakiwa kama ana sababu za msingi zitakazoifanya Mahakama hiyo isimpe adhabu kali kutokana na kosa linalomkabili.

Mshitakiwa aliomba aonewe huruma kwani ni mkosaji wa mara ya kwanza, na pia ana familia inayomtegemea.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Betraine alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John, iwapo anazo kumbukumbu kwa makosa ya zamani, na alijibu kuwa hana, ingawa aliomba itolewe adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 08/2020, Hakimu Betraine alisema amesikia maombi ya pande zote mbili, lakini kutokana na kubanwa na sheria kupitia vifungu 130 kifungu kidogo cha kwanza fungu la pili kipengele (e) pamoja na 131 fungu dogo la (1) na (3), alimhukumu kutumikia kifungo cha maisha gerezani.

Awali ilidaiwa na John, kuwa Januari 6, mwaka huu mchana, mshtakiwa alimbaka mtoto huyo, baada ya kufika nyumbani kwake akimuulizia rafiki yake na kujibiwa ametoka. Mwanasheria huyo alidai baada ya kumpa jibu hilo, mshtakiwa alimtaka mtoto huyo amsubiri akidai rafiki yake hachelewi, lakini wakati muathirika akiendelea kumsubiria mtoto mwenzake huyo, mshtakiwa alitumia mwanya huo kumshika na kumvutia chumbani kwake, kisha kumziba mdomo, kumvua nguo na kumbaka.

Pia, John alieleza baada ya kumaliza haja yake, mshtakiwa alimueleza mtoto huyo kutomueleza mtu yeyote.

Hata hivyo, mama mzazi wa mtoto huyo, alipombana mwanawe baada ya kutoridhishwa na hali yake, ndipo alipomtaja mtuhumiwa, hivyo mama alitoa taarifa kituo cha Polisi na kukamatwa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NO.** 263 **YA MWAKA** 2019

M. M. INDUSTRIES LTD **MDAI**

**DHIDI YA**

GREAT LAKES CONSTRUCTION CO. LTD **MDAIWA**

**KWA:**

MKURUGENZI MTENDAJI
Great Lakes Construction Co. Ltd
P.O.BOX 135,
MEATU

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 28/05/2020 saa **01.00. mchana**

**ANGALIA:**

Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 15/04/2020 **2020.**

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**KISUTU -DAR ES SALAAM**

21571/7102


# Mchakato wa utiaji nia udiwani, ubunge ACT leo

**Na Enock Charles**

CHAMA cha AC-Wazalendo, leo kinatarajia kutangaza utaratibu utakaotumika kupokea watia nia wa nafasi za ubunge na udiwani kupitia chama chicho katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema kuwa chama hicho kitakutana na wadau mbalimbali na kuweka mpango mkakati wa namna ya kuwapokea wote wenye nia ya kuwania nafasi za uongozi hasa katika ngazi ya ubunge na udiwani.

"Sisi bado lakini kesho (leo) ndio tutatangaza utaratibu kwa watia nia wa ngazi za ubunge na udiwani kuanza kujitokeza," alisema Ado.

Tayari chama kikuu cha upinzani nchini Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimefunga dirisha la watia nia kujitokeza Machi 30, huku ikielezwa kuwa watia nia zaidi ya watatu katika kila jimbo wamejitokeza ikiwemo 72 waliojitokeza katika majimbo yaliyopo katika Jiji la Dar es Salaam pekee.

Kati ya waliojitokeza kuwania nafasi hizo wapo waliojitokeza katika majimbo ambayo tayari yana wabunge wa upinzani kupitia chama hicho, huku baadhi ya viongozi walio katika nyadhifa mbalimbali katika chama hicho wakijitokeza pia kugombea katika majimbo.

Kwa pande wa nafasi ya Urais chama hicho kupitia Mkurugenzi wake wa Mambo ya Nje, Itikadi na Uenezi, John Mrema, kilisema hawajafungua milango, lakini kanuni za chama hicho zina ruhusu yeyote mwenye nia ya kugombea kiti hicho kumwandikia barua Katibu Mkuu wa chama hicho kuhusu nia yake.

# Wamiliki kampuni ukopeshaji washikiliwa kwa tuhuma nzito

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi, linawashikilia wafanyakazi na wamiliki wa kampuni 14 zinazojihusisha na utoaji mikopo kwa wananchi kwa tuhuma mbalimbali, zikiwamo kuendesha shughuli zao kinyume cha sheria.

Miongoni mwa madai hayo ni kutokuwa na vibali kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Lampuni hizo pia zinadaiwa kuhodhi kadi 607 za benki mbalimbali pamoja na vitambulisho viwili vya mpigakura kutoka kwa wateja wanaowapa mikopo.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Zambi alisema kukamatwa kwa wafanyakazi na wamiliki wa kampuni hizo kumetokana na wateja wanaowapa huduma ya mikopo kulalamikia riba kubwa wanazotozwa na masharti ya kuchukuliwa kadi zao za benki, huku wakilazimishwa kutoa namba zao za siri.

Alitaja kampuni ambazo wamiliki na wafanyakazi wake wanaoshikiliwa ni Mwema Credite Tanzania Ltd, Sumuni Credite, Mgunda Enterprises, William Credite, Febba Credite, Kimwecha Credite, Mtange Credite, Sado Finance Ltd, Platinam Credite, Mtange Investment, Maboto na Inas Credite, zote zipo Manispaa ya Lindi.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema kukamatwa kwa watumishi na wamiliki hao kumetokana na Ofisi yake kupokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wateja wao, hivyo kuanza kuzifuatilia ili kufahamu ukweli wake na kubaini kampuni sita zikihodhi kadi za benki za wateja 607 zikiwamo mbili za kupigia kura.

Alitaja idadi ya kadi zilizokuwa zinashikiliwa na kampuni hizo ni za benki za NMB (423), CRADB (106), Posta (50) na NBC (28), huku Mwema Credite Ltd inaongoza kwa kuwa na kadi (323) zikiwamo mbili za kupigia kura, ikifuatiwa na Mgunda Enterprises iliyo na kadi 132.

Kampuni zingine ni William Credite kadi 50, Febba Credite (41), Kimwecha (34) na Sumuni (32), na kwamba kati ya hizo (14) wenyeji Lindi zipo nne, Mwanzi mbili, Mtwara mbili na Mkoa wa Mara moja.

Zambi amesema kitendo cha wamiliki wa kampuni hizo kuchukuwa kadi za benki za wateja wao na mwisho wa mwezi kuchukuwa mishahara ni kinyume cha sheria ya nchi, kwani kadi na namba ya siri ni mali ya mwenye kadi.

Ofisa Biashara Mkoani Lindi, Victor Mimbi, alisema kampuni hizo licha ya kuwa na leseni za biashara, pia zinatakiwa kuwa na vibali viwili kutoka BoT na Wizara ya Viwanda na Biashara (Brela).

Baada ya maelezo hayo, Zambi alimuamuru Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Stanley Kulyamo, kuwafungulia kesi na kuwafikisha mahakamani, baada ya taratibu kukamilika.

## Takukuru yabaini vyanzo vya upotevu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Pwani, imesema kutokuwa na wataalamu wa fedha kwenye vyama vya msingi ni moja ya chanzo cha upotevu ama ubadhilfu wa fedha kwenye vyama hivyo.

Hayo yamebainishwa juzi mjini Kibaha na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusiana na shughuli zilizofanywa na Taasisi hiyo.

Suzana alisema, katika kipindi cha miezi mitatu walifanyaa uchambuzi katika mifumo 13 kwenye vyama vya msingi na miundombinu ya barabara inayosimamiwa na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (Tarura).

Alisema, kwa upande wa vyama vya msingi (AMCOS), walibaini vingi kutokuwa na wataalamu wa fedha hivyo miongoni mwa wanachama kutumika kama wahasibu.

Mkuu huyo wa Takukuru alisema, hali hiyo ni changamoto kwa kuwa wengi wao hawatunzi kumbukumbu za mahesabu na kusababisha upotevu wa fedha.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Klabu ziingie sokoni kusaka wadhamini

**LIGI** Kuu Tanzania Bara kwa sasa imesimama kama zilivyo ligi mbalimbali barani Afrika, Asia, Ulaya na kwingineko kutokana na mlipuko wa janga la virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19 ambao unaua maelfu ya watu duniani.

Kwa Tanzania, hadi jana mchana bado watu waliothibitika kuambukizwa walikuwa 299 kati yao 48 wakielezwa kupona na vifo vikiwa 10 pekee, wakati kwa dunia nzima kulikuwa na maambukizi 2, 923,656, waliopona 837,609 na vifo jumla vikiwa 203,317.

Kasi hiyo ya maambukizi na vifo vilivyotokana na virusi hivyo vilivyoanzia mjini Wuhan, China Desemba mwaka jana, ndiyo iliyosababisha mchezo pendwa duniani wa soka na mingine mingi kwenda likizo kwa kipindi kisichojulikana.

Kusimama huko kwa ligi kumeziathiri klabu nyingi duniani zikiwamo kubwa za Ulaya, Barcelona ikiwa ni mojawapo ambayo wachezaji wake wamekubali kukatwa sehemu ya mishahara yao ili kuiwezesha kuwalipa wafanyakazi wasio wachezaji.

Lakini pia jana Klabu ya Aston Villa ya England anayoichezea nahodha na mshambuliaji wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, nayo ilitangaza wachezaji wake, benchi la ufundi na viongozi wa juu kukubali kukatwa asilimia 25 ya mishahara yao kwa kipindi cha miezi minne ili kuisaidia klabu kujiendesha katika kipindi hiki ambacho janga la corona linaendelea kuitesa pia nchi hiyo wakati huu ikiwa na wagonjwa 148,377 huku watu 20,319 wakiwa wameshapoteza maisha kutokana na COVID-19.

Na katika kuonyesha ni kwa namna gani Rais wa Shirikisho la Soka duniani (Fifa), Gianni Infantino anatambua athari kubwa iliyosababishwa na virusi vya corona kwa kurudisha nyuma maendeleo ya soka, ametangaza kutoa Dola za Marekani milioni 150 sawa na Sh. bilioni 344.8 za Tanzania kwa ajili ya kuzigawa kwa wanachama wake 211 Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ikiwa miongoni mwao, lengo likiwa ni punguza athari zilizojitokeza.

Kwa mgawo huo, kila mwanachama wa Fifa atapata dola 500,000 sawa na Sh. bilioni 1.14 za Tanzania, jambo ambalo tayari baadhi ya klabu zimeanza kuzitolea macho wakati ikiwa bado haijulikani TFF itazielekeza upande gani.


Hii ni kutokana na baadhi ya klabu za Tanzania kwa kipindi hiki kifupi tu cha janga hili, kushindwa kuwalipa wachezaji na makocha wao mishahara kutokana na kutegemea zaidi mapato ya mlangoni ili kujiendesha. Tunaamini huu si wakati wa klabu kuendelea kutegemea mapato ya mlangoni ama kutupia jicho migawo kama hiyo ya Fifa, na badala yake tulitarajia kusikia angalau viongozi wa klabu hizo wakiketi kitako na wachezaji na kuwaomba kupunguziwa asilimia kidogo ya mishahara yao kama ambavyo wenzao wa Ulaya wanafanya kwa sasa.

Lakini hilo limeshindikana kutokana na klabu nyingi za Tanzania kutokuwa na wadhamini wakutosha kutoa fungu la haja linaloweza kukidhi mahitaji angalau ya kulipa mishahara ya wachezaji. Lakini pia, tunashangazwa na baadhi ya viongozi kuanza kusingizia janga la corona kuwa sababu ya kushindwa kuwalipa mishahara wachezaji wake, wakati kwa zingine hata kabla ya mlipuko wa virusi hivyo bado suala la kulipwa mishahara lilikuwa tatizo kubwa kwao. Hivyo, huu ni wakati sasa kwa viongozi wa klabu kuanza kujipanga na kuingia sokoni kusaka wadhamini na si kuwatafuta tu bali pia kuheshimu mikataba wakayoingia ili kuilinda na kuzisaidia kujiimarisha kiuchumi kwa msimu ujao.

Ni wazi makocha wamekuwa wakitoa programu mbalimbali za mazoezi kwa njia ya mtandao ili kuwawezesha wachezaji wao kujiweka fiti tayari kwa kurejea dimbani siku yoyote serikali itakapotangaza michezo kuendelea pale hali ya mlipuko wa virusi hivyo itakapotulia ama kupatikana dawa.

Jambo ambalo linaonekana itakuwa ni vigumu kwa baadhi ya wachezaji hao kuweza kutekeleza programu hizo za mazoezi kutokana na kuelekeza akili zao katika kutafuta fedha za kujikimu katika kipindi hiki ambacho klabu zao zinashindwa kuwalipa kwa wakati. Ifahamike, lengo letu ni kuona Ligi Kuu Bara ikiwa miongoni mwa ligi bora tatu barani Afrika zenye ushindani mkubwa zaidi, na hilo litafanikiwa tu endapo viongozi wa klabu watahakikisha wanazijengea uchumi imara utakaowawezesha kuwalipa vizuri na kwa wakati wachezaji wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Tukipunguza wageni Kombe la Afrika ni ndoto

Na Adam Fungamwango

**HUWA** sielewi Watanzania nini tunahitaji ili soka nchi hii liendelee na kutuletea mafanikio kwenye ngazi ya klabu na hata timu za Taifa.

Nimesikia majuzi mjadala wa wachezaji wa kigeni ukitinga mpaka bungeni, baadhi wakiujadili. Nilishangaa mjadala huu kurudi tena kwa sababu ulishamalizika na wadau wengi wakapendekeza kuwa wachezaji wa kigeni idadi yao kusajiliwa na klabu moja ibaki kuwa 10 tu.

Ukiusikiliza mjadala huu wakati mwingine unabaki unacheka kwa sababu hata wenyewe wanaoujadili wanajichanganya.

Wanaotaka wachezaji wapunguzwe wana hoja mbili ambazo huwa wanazisimamia sana. Ya kwanza ni kwa kulinda vipaji vya wacheza wa Kitanzania. Yaani wageni wanazuia vipaji vya vijana kuonekana.

Hoja ya pili wanaopinga wageni, ni kwamba wachezaji wanaokuja hapa nchini baadhi viwango vyao ni vya chini, hivyo wanataka viwekwe vigezo ili kupata wachezaji wenye uwezo mkubwa, na wanaotaka wasajiliwe ni wale wanaocheza timu za taifa za nchi husika.

Sasa hapo unajiuliza, hawa tu waliopo ambao wanadaiwa wengine viwango vyao cha chini wanaambiwa wanazuia vipaji vya Watanzania kuonekana, wakija hao wenye vigezo vikubwa hawa Wabongo watapata namba kweli?

Hivi kama wa Kibongo anawekwa benchi na David Molinga ambaye hachezi timu ya Taifa ya DR Congo, sasa akiletwa anayecheza timu ya taifa, nani atapata namba?

Inachekesha kuwa vigezo vinavyosemwa na baadhi ya wadau vitumike, vinamtoa mpaka Bernard Morrison kucheza Ligi Kuu ya Tanzania, kwa sababu haichezei timu ya Taifa ya Ghana.

Hivi kweli ligi yetu inaweza kuwa ni bora kiasi cha kumfanya mchezaji kama Morrison asiwe na kigezo cha kuichezea?

Ili wachezaji wetu wajitume wanahitaji changamoto za kushindana na wachezaji wa kigeni na si kuwawekea mazingira mepesi ya kupambana.

Inashangaza kuona wachezaji zaidi ya 600 wa Kitanzania, eti wanatafutiwa kanuni, kupunguza wachezaji wasiozidi 50 tu wa kigeni. Ni aibu kubwa.

Timu zinazosajili wachezaji wa kigeni wengi ni tatu tu, Simba, Yanga na Azam, zingine zinasajili watatu, wawili, au mmoja na zingine hazisajili kabisa, tutasemaje Wabongo wanabanwa?

Na hizo kanuni za kuwapunguza ni kwamba zitakuwa zinawekwa kwa ajili ya Simba, Yanga na Azam tu.

Simba, Yanga na Azam ni klabu ambazo lengo lao ni kucheza mechi za kimataifa, kuingia makundi ya Ligi ya Mabingwa na hatimaye kutwaa Kombe la Afrika na makombe mengine, suala la kukuza soka la Tanzania ni la nchi nzima na si la timu hizo tu kupangiwa wachezaji wa kuwa nao.

Kwa wachezaji hawa wa Kitanzania, tusidanganyane kama hizi timu zinaweza hata kuingia makundi tu.

Tukumbuke kuwa Mtibwa Sugar msimu uliopita ilitolewa mapema na KCCA ya Uganda Kombe la Shirikisho, ikafungwa nje ndani kwa sababu haikuwa na wachezaji wa kimataifa, na kama ingekuwa nao, mechi ilikuwa rahisi tu kwao.

Simba iliingia robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na ilichangiwa kiasi kikubwa na wachezaji wa kigeni kina James Kotei, Claotus Chama, Meddi Kagere, Emmanue Okwi, wakisaidiwa na Wabongo waliopambana kutapata namba, kina John Bocco, Kapombe na wengineo.

Msimu huu KMC FC haikufua dafu kwenye Kombe la Shirikisho Afrika kwa sababu hiyo hiyo, lakini ikumbukwe Yanga ilitolewa kwa mbinde na Zesco ya Zambia, almanusura itinge hatua ya makundi, hii yote ilitokana na kuwapo kwa wachezaji wa kigeni, kina Tshishimbi, Juma Balinya, Sadney Urkhob. Tusijidanganye wachezaji wa kigeni ni muhimu sana na wachezaji wa Kitanzania wanatakiwa wapitia kwenye hatua ngumu ili wawe wachezaji wazuri na kupata namba mbele ya wachezaji na si kuwadekeza.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU

### HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA, MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21



***Mhe. Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb.)***
***Waziri***



***Mhe. William Tate Ole Nasha (Mb.)***
***Naibu Waziri***



***Dkt. Leonard Douglas Akwilapo***
***Katibu Mkuu***



***Profesa. James Epiphan Mdoe***
***Naibu Katibu Mkuu***



***Dkt. Ave Maria Semakafu***
***Naibu Katibu Mkuu***

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NATEKNOLOJIA, MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21 DODOMA APRILI, 2020

**A. UTANGULIZI**

**1.** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**2.** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutimiza majukumu yetu hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa letu na Dunia kwa ujumla inakabiliwa na janga la ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu inayotokana na virusi vya Corona (COVID-19). Kwa namna ya pekee na kwa unyenyekevu mkubwa, natoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuendelea kuniamini katika dhamana ya kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa moyo wa dhati, kwa umakini na uadilifu wa hali ya juu, huku nikimtanguliza Mwenyezi Mungu mweza wa yote.

**3.** Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, kwa uongozi wake thabiti na kwa uzalendo alionao katika kulinda na kusimamia rasilimali za nchi yetu. Watanzania wanashuhudia miradi mikubwa ya maendeleo ikitekelezwa katika sekta zote muhimu. Tuendelee kumuunga mkono ili aendelee kufanikisha azma yake ya kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu.

**4.** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), kwa uongozi wao makini. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliotukuka.

**5.** Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze kwa dhati wewe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri wa hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya.

**6.** Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020. Marehemu Rwakatare alikuwa ni mmiliki wa Shule za St. Mary's na pia mmiliki wa Chuo cha Ualimu cha St. Mary's kilichopo Tabata. Ni dhahiri kuwa, Wizara imepoteza mdau muhimu sana katika Sekta ya Elimu. Mchango wake katika kutoa elimu nchini tutaendelea kuuthamini na kuuenzi. Pia natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**7.** Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa shule pamoja na vyuo vimefungwa ikiwa ni hatua ya Serikali kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Corona. Wizara yangu imeanzisha vipindi maalum vya Redio na Televisheni ili wanafunzi waendelee kupata elimu wakiwa nyumbani. Hivyo, natoa wito kwa Wazazi na Walezi kuendelea kuwasimamia Watoto wao ili kuhakikisha wanaendelea kujisomea. Aidha, nawasihi waendelee kuwakinga na wasiwaruhusu kutoka nyumbani bila kuwa na sababu za msingi. Napenda pia kuwasihi wanafunzi, walimu na wadau wote wa elimu kwa ujumla, kuendelea kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Wataalam wa Afya ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa Corona.

**8.** Mheshimiwa Spika**,** Naomba kutoa shukrani za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb), na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na mapendekezo yao, ambayo yamechangia kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri mlionipa kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**9.** Mheshimiwa Spika**,** naishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu hayo kwa utulivu.

**10.** Mheshimiwa Spika**,** baada ya maelezo hayo sasa naomba nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

**11.** Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,386,508,723,272.00** kwa ajili ya Fungu 46. **Shilingi 523,788,923,012.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 862,719,800,260.00** za Miradi ya Maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - Fungu 18, Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,156,017,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na mishahara ya watumishi wa Tume.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

**12.** Mheshimiwa Spika**,** Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 553,739,899,119.13**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 335,148,981,970.31** sawa na asilimia **60.5** ya Makadirio.

**13.** Mheshimiwa Spika**,** Kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 27,000,000.00**; na imekusanya **Shilingi milioni 8.5** hadi kufikia mwezi Machi, 2020.

**Matumizi ya Kawaida**

**14.** Mheshimiwa Spika**,** Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 396,788,907,260.36** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia **75.8** ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18, Wizara ilipokea **Shilingi 1,176,454,000** sawa na asilimia **54.56** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Miradi ya Maendeleo**

**15.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 30, 2020 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 734,890,659,288.20** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

ni sawa na asilimia **85.20** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU**

**16.** Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20.

**Uongezaji Fursa za Upatikanaji Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu**

**17.** Mheshimiwa Spika**,** Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali:

(i) imewezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 9,712, matanki ya maji 911 pamoja na miundombinu ya kunawia mikono katika shule za msingi 602 kupitia **Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni.**

(ii) imesajili jumla ya shule 395 zilizokidhi vigezo kati ya 407 zilizoomba;

(iii) imetoa jumla ya leseni 253 za kufundishia;

(iv) imenunua na kusambaza vifaa maalum vya kielimu katika shule maalum na vitengo 424 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(v) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 269 wa sekondari kuhusu matumizi ya Lugha ya Alama.

Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu

**18.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali inatambua umuhimu wa walimu katika kuinua ubora wa elimu nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali:

(i) imeimarisha elimu ya michezo ikiwa ni pamoja na kuendesha mashindano ya michezo na sanaa katika Vyuo vya Ualimu (UMISAVUTA);

(ii) imenunua magari 39 kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R, ambapo magari 35 yamegawiwa katika Vyuo vyote vya Ualimu vya Serikali na magari 4 ni kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini;

(iii) imesambaza aina 449 za vitabu zenye jumla ya nakala 25,709 kwa ajili ya masomo yote yanayofundishwa vyuoni;

(iv) imenunua na kusambaza katika Vyuo vya Ualimu kompyuta 480, UPS 480, photocopy machines 35, kompyuta mpakato 43, na servers 2 ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA;

(v) imetoa mafunzo kazini ya TEHAMA kwa wakufunzi 530;

(vi) imetoa mafunzo kazini ya TEHAMA na teknolojia saidizi kwa Walimu 125 na Wakufunzi 9 wenye mahitaji maalum; na

(vii) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 771 katika Halmashauri 20 zenye ufaulu wa chini katika somo la Hisabati.

Kusimamia Ubora wa Elimu katika Shule na Vyuo vya Ualimu

**19.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zilizopata Ithibati na Usajili zinatoa elimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali:

(i) imefanya tathmini ya mazingira ya utoaji wa elimu katika asasi 4,102;

(ii) imefanya ukaguzi maalum katika asasi 548;

(iii) imeongeza Wathibiti Ubora wa Shule wapya 400 katika ofisi za Kanda na Wilaya;

(iv) imekamilisha ujenzi wa ofisi mpya 100 za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya zilizogharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 15.2;**

(v) imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(vi) imewezesha vijana 2,534 kupata mafunzo ya uanagenzi.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**20.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Juu kama nyenzo muhimu ya kuifikisha nchi yetu katika uchumi wa kati, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali:

(i) imeendelea kugharamia wanataaluma 620, ambapo 196 ni wa Shahada ya Umahiri, na 424 Shahada ya Uzamivu kwa lengo la kuwa na wahadhiri waliobobea katika fani zao;

(ii) imeratibu ufadhili nje ya nchi wa wanafunzi 115 wa Kitanzania;

(iii) imefadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(iv) imefadhili wanafunzi 207 (Umahiri 107 na Uzamivu 100) kupitia Mradi wa Vituo vya Umahiri vya Africa.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**21.** Mheshimiwa Spika, katika kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini, Serikali:

(i) imetambua na kuhakiki teknolojia 231 zilizozalishwa nchini kwa lengo la kuwa na kanzidata ya kitaifa;

(ii) imepata ufadhili wa jumla ya **Euro 965,220** sawa na **Shilingi 2,414,045,190.13** kwenye miradi mipya mitano (5) ya utafiti katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo; na

(iii) imewaendeleza wabunifu 60 waliopatikana katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka 2019. Aidha, bunifu za wabunifu 12 zipo katika hatua ya kutengeneza bidhaa za mfano (prototypes) tayari kwa kuingia sokoni.

**SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI, MAMLAKA NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**22.** Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu majukumu ya Taasisi, Mamlaka na Wakala zilizo chini yake ili kuhakikisha nchi inazalisha rasilimaliwatu yenye weledi kwa kuzingatia mahitaji ya nchi, Soko la Kikanda na Kimataifa. Shughuli zilizofanyika kwa kila Taasisi zimeainishwa kwa kirefu katika kitabu cha Hotuba. Nitaeleza kwa kifupi baadhi ya shughuli.

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**23.** Mheshimiwa Spika**,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20 Serikali, kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:

(i) kimekarabati Bweni Na. 1 Kitalu G linalotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalum lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 63, pamoja na ukarabati wa

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

majengo ya Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia;

(ii) kimeendelea na ukarabati mkubwa wa mabweni Namba 2 na 5 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 788 ambayo yakikamilika yatakiwezesha chuo kufikia jumla ya wanafunzi 11,103 wanaopata malazi katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere;

(iii) kimeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la kituo cha wanafunzi kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi;

(iv) kimeendelea na ujenzi wa mfumo mpya wa maji katika Kampasi ya Mwl. J.K. Nyerere unaohusisha kuweka upya mabomba makubwa mapya, kujenga tanki la maji lenye mita za ujazo 500,000, na kufunga mashine kubwa zitakazowezesha kusafirisha maji kiasi cha lita 360,000 kwa saa.

**Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**24.** Mheshimiwa Spika**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, imetekeleza yafuatayo:

(i) imeanzisha kampasi mpya katika Mkoa wa Katavi iliyopewa jina la Waziri Mkuu mstaafu Mhe. Mizengo Peter Kayanza Pinda ambayo itatoa masomo ya Stashahada, Astashahada na Shahada katika nyanja za Kilimo na Mifugo;

(ii) imeimarisha Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza, kumbi za mikutano na Idara ya Huduma za Afya;

(iii) imejenga jengo la Maabara Mtambuka lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja kwa gharama ya **shilingi bilioni 11.5**; na

(iv) imekamilisha ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu.

**25.** Mheshimiwa Spika**,** Chuo kimeboresha shamba darasa kwa ajili ya kupanda mazao ya Taifa ya kimkakati. Uboreshaji wa shamba hilo umechochewa na uwepo wa matrekta 10 yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, baada ya kutembelea Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine mnamo tarehe 07 Mei, 2018. Aidha, chuo kimeboresha shamba darasa kwa kufunga vifaa vya kisasa vya kilimo na kupanda mazao ya kitaifa ya kimkakati kama vile zabibu, pamba, katani, kakao, kahawa, mananasi, migomba na mazao ya mbogamboga.

**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili** kinaendelea na ujenzi wa kituo cha Umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu - Center of Excellence in Cardiovascular Sciences.

**Chuo Kikuu cha Ardhi**

(i) kimeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kuhusu usanifu majengo, utayarishaji wa mipango ya kuendeleza miji na uthamini; na

(ii) kinaendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 ili kuongeza sehemu za malazi.

**Chuo Kikuu Mzumbe** kimeendelea na ujenzi wa madarasa na kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na ofisi zenye uwezo wa kuchukua wafanyakazi 50 katika Kampasi Kuu.

**Chuo Kikuu cha Dodoma** kinaendelea na ujenzi wa jengo la kitengo cha huduma za mionzi katika hospitali ya chuo kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji huduma.

**Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

(i) kimetoa mafunzo kwa vyama 101 vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) katika wilaya 61 za Tanzania Bara;

(ii) kimefanya ukarabati na upanuzi wa mabweni 9, hivyo kuongeza nafasi za malazi 460; na

(iii) kimekamilisha ujenzi wa kafteria yenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja.

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

(i) kimeimarisha mtandao wa kujifunzia kwa njia ya masafa kwa kutengeneza programu mpya 35 ambapo 30 zilipitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu; na

(ii) kimeimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kuzindua maabara tatu (3) za Sayansi.

**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia** kimeendelea na jitihada za upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo ya chuo.

**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)**

**26.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali imeendelea kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ufundi kupitia Chuo cha Ufundi Arusha, Serikali:

(i) imeendelea na ukarabati wa nyumba 68 za watumishi, na ukarabati wa mabweni matatu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800;

(ii) imekamilisha ujenzi wa jengo la kufundishia kuhusu matumizi ya nishati jadidifu ya umeme wa jua; na

(iii) inaendelea na ujenzi wa miundombinu katika Kituo cha Mafunzo ya Nishati Jadidifu (Renewable Energy) cha Kikuletwa.

**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere** kimeendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika kampasi ya Zanzibar lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha malazi kwa wanafunzi.

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**

(i) Mheshimiwa Spika**,** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi ili kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata Stadi, Ujuzi na Maarifa stahiki. Katika mwaka 2019/20 Taasisi imeboresha Mkakati wa Kuendeleza Kisomo na Elimu kwa Umma ili uendane na mahitaji ya sasa.

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**27.** Mheshimiwa Spika**,** Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya,

(i) kimeendelea na ujenzi wa maktaba itakayogharimu kiasi cha **Shilingi 5,523,685,496.00** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja;

(ii) kimekamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja; na

(iii) kimekarabati ofisi 80 na hivyo kuongeza nafasi za ofisi kwa

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

wafanyakazi 320.

(i) kimeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii na kushiriki katika kupima ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi miwili mikubwa ya kimkakati ambayo ni mradi wa kufua umeme wa maji (Julius Nyerere Hydropower Project) na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway).

**Baraza la Mitihani la Tanzania - NECTA**

**28.** Mheshimiwa Spika**,** Baraza la Mitihani la Tanzania limekamilisha Uchapaji, Usafirishaji na Usahihishaji wa mitihani ya Kitaifa ya Darasa la Nne, Kidato cha Pili, Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE), Mitihani ya Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa (QT).

**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania – TCU**

(i) imeratibu maombi 99,014 ya wanafunzi walioomba kujiunga na masomo kwa mwaka 2019/20;

(ii) imeandaa Mwongozo wa waombaji wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi ili kuhakikisha wanaenda kusoma katika vyuo vinavyotambulika; na

(iii) imechapisha kitabu kinachoeleza "Hali ya Elimu ya Juu nchini, 2018" ili kutoa taarifa mbalimbali kuhusu Elimu ya Juu.

**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**

**29.** Mheshimiwa Spika**,** Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi,

(i) limefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya ufundi 109; na

(ii) limetoa mafunzo kuhusu Mitaala inayozingatia Umahiri kwa wakufunzi 608 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi.

**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)**

**30.** Mheshimiwa Spika**,** kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Taasisi ya Elimu Tanzania,

(i) imekamilisha uandishi, uchapaji na usambazaji wa aina nane za vitabu vya kiada vya Darasa la VI ambapo jumla ya nakala 2,962,155 zimesambazwa katika Halmashauri zote nchini;

(ii) imeandaa na kusambaza nakala 272,000 za Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo yote nane;

(iii) imechapa na kusambaza nakala za vitabu 1,359,350 vya masomo yote kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi, Darasa la I-V kwa shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia;

(iv) imechapa na kusambaza nakala 719,905 za vitabu vya kiada vya Elimu ya Awali na nakala 41,642 za Mwongozo wa Mwalimu wa kufundishia Elimu ya awali;

(v) imechapa na kusambaza nakala 1,567,537 za aina 15 ya vitabu vya Sekondari;

(vi) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na vya maandishi ya Nukta Nundu kwa ajili ya wanafunzi wasioona; na

(i) imetoa mafunzo kabilishi kwa walimu 592 wa Shule zisizo za Serikali kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi; na walimu 431 wa Sekondari yaliyolenga kuwawezesha kutekeleza kwa ufanisi mtaala ulioboreshwa.

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**

**31.** Mheshimiwa Spika**,** Mamlaka ya Elimu Tanzania,

(i) inaendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 katika shule za msingi 22 na shule za sekondari tano (5) zenye uhitaji mkubwa;

(ii) inaendelea na ujenzi wa mabweni 16 ya wasichana katika shule 16 za sekondari;

(iii) inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 40 za walimu; na

(iv) inaendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 528 kwenye shule zenye uhitaji mkubwa.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**32.** Mheshimiwa Spika**,** Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu,

(i) umetoa Mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) umetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Taaluma kwa wajumbe 245 wa Menejimenti za Vyuo vya Ualimu;

(iii) umetoa mafunzo kwa Maafisa Elimu 383 ngazi ya Mkoa na Wilaya ili kuboresha utendaji wao; na

(iv) umetoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Sekondari pamoja na Maafisa Elimu Kata 985.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**33.** Mheshimiwa Spika**,** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi 132,119 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 449.99**; na

(ii) imeendelea na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 144.3** kati ya **Shilingi bilioni 166.1** zilizolengwa kukusanya hadi Machi 2020 zilikuwa zimekusanywa.

**Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)** imewezesha upatikanaji wa jumla ya vitabu 310,490, magazeti na majarida 4,906 kwa ajili ya kuwaongezea wasomaji makala mbalimbali.

**Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC)** imeendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili ambayo inagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 10.4.**

**B. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 itatekelezwa kupitia Idara, Vitengo na Taasisi .

**Baraza la Mitihani la Tanzania** litaendelea na upimaji wa Mitihani ya Kitaifa.

**Taasisi ya Elimu Tanzania** itaendelea na uchapaji na usambazaji wa vitabu na miongozo**.**

**35.** Mheshimiwa Spika**,** Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Wakala wa Maendeleo

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

ya Uongozi wa Elimu, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) zitatekeleza majukumu kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha Hotuba.

**Elimu ya Juu**

Taasisi za Elimu ya Juu zitaendelea na majukumu yao ya kudahili wanafunzi, kufanya tafiti na kutoa huduma kwa jamii. Aidha, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu itatoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji 54,000 wa mwaka wa kwanza ikilinganishwa na wanafunzi 49,799 wa mwaka wa kwanza wanaonufaika kwa mwaka 2019/20.

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam** kitakamilisha upanuzi wa Hosteli za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongeza ghorofa mbili zaidi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 na hivyo kufanya Hosteli hizo kuweza kuchukua jumla ya wanafunzi 5,120. Aidha, chuo kitajenga jengo la Shule Kuu tarajiwa ya Uchumi katika kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lenye ghorofa sita (6).

**USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA**

**36.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Wizara itatekeleza miradi ambayo ni pamoja na:

(i) Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Programme for Results – EP4R);

(ii) Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ);

(iii) Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu;

(iv) Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(v) Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP);

(vi) Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC);

(vii) Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni;

(viii) Mradi wa Kuimarisha Ubora Elimu ya Sekondari – SEQUIP; na

(ix) Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki (East Africa for Transformation and Regional Integration Project - EASTRIP).

**TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**37.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itatekeleza shughuli kama zilivyoainishwa katika kitabu cha Hotuba.

**C. SHUKRANI**

**38.** Mheshimiwa Spika, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa William Tate Olenasha (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo, na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao wa karibu katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

**39.** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Walimu, Wanafunzi na Wadau wa Elimu, kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki wa Shule, Vyuo na Taasisi Binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika utoaji wa elimu hapa nchini.

**40.** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Elimu wote ambao wamechangia kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**41.** Mheshimiwa Spika, napenda pia kuyashukuru mashirika yaliyochangia kufanikisha programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo yameainishwa katika Kitabu cha Hotuba. Tunawashukuru sana.

**D. MAOMBI YA FEDHA WA MWAKA 2020/21**

**42.** Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo ya mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,348,563,375,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

**(i)** **Shilingi 491,049,151,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara;

**(ii)** **Shilingi 857,514,224,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 606,715,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 250,799,224,000.00** ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba jumla ya **Shilingi 2,239,181,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa, naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara Mafungu yote mawili (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 1,350,802,556,000.00.**

**45.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni http://www.moe.go.tz.

**47.** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

# Mwanajeshi jela miaka mitatu kwa kujeruhi

**Na Said Hamdani,** LINDI

ASKARI wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikosi cha KJ 843, wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, MT 92665 Coplo Shabani Mkondya (34), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu gerezani, baada ya kukutwa na hatia ya kumjeruhi mkazi wa Kata ya Nyangao, Ramadhani Mussa, kutokana na wivu wa mapenzi.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Maria Batraine, baada kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshitakiwa alipewa nafasi ya kujitetea, na kuiomba Mahakama hiyo isimpe adhabu kali kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza, na pia alilazimika kufanya hivyo, baada ya kuzidiwa na hasira kutokana na kitendo alichofanyiwa na mlalamikaji.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batraine alimuuliza Mwanasheria wa jamhuri, Emmanuel John, iwapo ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu kuwa hana.

Hata hivyo, John aliomba adhabu kali itolewe kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo, ikizingatiwa yeye ni mlinzi wa umma.

Hakimu Betraine akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 61/2019, kupitia kifungu cha Sheria namba 225 kanuni ya adhabu sura ya 16/2002, alisema amesikia maombi ya pande zote mbili, na kumhukumu kifungo cha miaka mitatu gerezani.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na John kwamba, mshtakiwa alimjeruhi sehemu mbalimbali za mwili wake, Mussa, baada ya kumfumania kwa mchumba wake (jina limehifadhiwa).

John alieleza kwamba mshtakiwa alifanya kitendo hicho, Kata ya Nyangao, Halmashauri ya Wilaya na Mkoa wa Lindi, Agosti 8, 2019 majira ya usiku.

**Hakimu Betraine akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 61/2019, kupitia kifungu cha Sheria namba 225 kanuni ya adhabu sura ya 16/2002, alisema amesikia maombi ya pande zote mbili, na kumhukumu kifungo cha miaka mitatu gerezani.**

# Kanisa kutoa barakoa kwa waumini wake

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

PAROKIA ya Mt Vicent wa Paulo Katubuka Jimbo la Kigoma, imeweka mkakati wa kila muumini na familia yake kupata barakoa mbili za kufua ili kuwezesha kujikinga na ugonjwa wa virusi vya corona.

Akielezea hatua hiyo, Paroko wa Parokia hiyo, Padre Stephene Shaiju, wakati wa misa takatifu jana iliyoambatana na utolewaji wa elimu ya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo, alisema wameamua kuweka mkakati wa kuunganisha nguvu zao pamoja ili kuwawezesha waumini na familia zao kujikinga wanapokuwa kanisani na sehemu zingine.

Padre Shaiju alisema kwa uhalisia vipato vya wengi havimudu gharama za ununuzi wa barakoa, hivyo mpango huo utawezesha mwenye uwezo kutoa fedha, vifaa kama cherehani za kushonea na wenye ujuzi wa kushona pia kujitolea kufanya kazi hiyo na baadaye vifaa kinga hivyo vitagawiwa kwa waumini wote.

"Inabidi tuunganishe nguvu kwa pamoja katika hili ili kusaidiana, mwenye cherehani alete, mwenye uwezo wa kununua vitambaa alete na masisita wetu watatuelekeza namna ya kushona barakoa, lakini pia daktari atatuelekeza kitambaa sahihi kinachokidhi vigezo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Hospitali ya Kabanga, wilayani Kasuku, Dk. Peter Mayengo, akitoa maelekezo ya kitalamu ya namna ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo, alisema wananchi wanapaswa kutopuuza maelekezo yanayotolewa na serikali kupitia watalamu wa afya.

Daktari Mayengo alisema baadhi ya mambo muhimu ambayo kila mtu anapaswa kuyazingatia kuwa ni kuacha mikusanyiko isiyo ya lazima, kutumia barakoa, kunawa mikono kwa kutumia sabuni na maji tiririka kwa sekunde zisizopingua 20 kutojigusa katika maeneo ya uso ambayo ni macho na pua.



Mafundi wakijenga moja ya madarasa mapya ya Shule ya Msingi Nyamiyenga iliopo Kata ya Kiriba wilaya ya Musoma mkoani Mara juzi ikiwa ni uboreshaji wa miundombinu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Raia wa Nigeria mahakamani kwa madai ya uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Nigeria David Chukwu (38) na wenzake wawili wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na kesi ya Uhujumu Uchumi ikiwa kusafirisha kilo 268.50 za dawa za kulevya na kutakatisha fedha.

Washtakiwa hao walisomewa Mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Godfrey Isaya.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Veronica Matikila, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali, Batilda Mushi.

Mushi aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni, Isso Lupembe (49) Mkazi wa Mbezi na Allistair Mbele (38), mkazi wa Mbezi Kibanda cha Mkaa.

Alidai kuwa Aprili 15, mwaka huu eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa, washtakiwa wote kwa pamoja walikutwa wakisafirisha kilo 268.50 dawa za kulevya aina ya heroine.

Wankyo alidai katika shtaka la pili kuwa, kati ya Januari Mosi, 2016 na Aprili 15, mwaka huu washtakiwa walitakatisha fedha baada ya kujihusisha na miamala ya Dola za Marekani 61,500 na Sh. 17,835,000 huku wakijua ni zao la tangulizi la biashara ya dawa za kulevya.

Matikila alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Pia, alidai kuwa upande wa Jamhuri umefanya juhudi za kuwapima washtakiwa virusi vya Corona kwa sababu wanakabilika na mashtaka ambayo hayana dhamana.

"Mheshimiwa hakimu tumewapima washtakiwa afya zao kujua kama wana maambukizi ya virusi vya Corona au la, majibu yao ni negative (hasi) kuonyesha kwamba tuko makini kupelekea mahabusu walio salama.

Hakimu Isaya alisema Jamhuri wamefanya vizuri kuwapima Washtakiwa afya zao, kesi itatajwa Mei 8, mwaka huu washtakiwa wapelekwe mahabusi.

# WAFUNGAJI WA5 WA WAKATI WOTE LIGI KUU



MMACHINGA

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA inaonyesha kuwa mfumo wa Ligi Tanzania Bara uliozishirikisha timu zote Bongo ulianza rasmi mwaka 1965, kabla ya hapo ligi ilikuwa ikichezwa mkoani Dar es Salaam tu.

**Tangu mwaka huo wa kwanza ambapo timu ya Sunderland kwa sasa Simba ilipoweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kutwaa ubingwa ulioshirikisha timu zote Tanzania, kuna baadhi ya wachezaji wameweka rekodi mbalimbali, ikiwamo kuwa wafungaji bora wa msimu.**

Hata hivyo, kuna baadhi ya wachezaji wameweka rekodi za aina yake ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja wa ligi, huku wakitwaa Kiatu cha Dhahabu.

Kwa miaka ya hivi karibuni kuna baadhi ya wachezaji wamekuwa wakionekana kutishia kuivuka rekodi ya kufunga mabao mengi, ingawa imekuwa ngumu kidogo.

Kwenye makala haya, mwandishi amekusanya rekodi za wachezaji waliowahi kuwa wafungaji wa wakati wote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa idadi kubwa ya mabao yanayoingia kwenye rekodi ya soka la Bongo.

**1. MOHAMED HUSSEIN 'MMACHINGA'-YANGA (MABAO 26)**

Huyu ndiye mfungaji bora wa muda wote kwenye soka la Tanzania tangu Ligi Kuu ianze mwaka 1965 kwa kufunga mabao mengi zaidi kuliko mtu mwingine yeyote.

Mohamed Hussein maarufu kama 'Mmachinga' ni Mtanzania ambaye rekodi yake inaendelea kuwapo hadi leo, ikiwashinda hata wachezaji wengi wa kigeni ambao wakati mwingine wamekuwa wakikaribia zaidi kuifikia.

Aliiweka mwaka 1997, akifunga mabao 26, akiifanya timu yake ya Yanga kutwaa ubingwa kwa pointi 44, ikiipiku Simba iliyomaliza ikiwa na pointi 38, akiwa mfungaji bora msimu huo.

Kwenye ligi hiyo, Yanga ilifunga mabao 30, ikiwa na maana kuwa ni manne tu ambayo yalifungwa na wachezaji wengine msimu mzima, kukiwa na timu 12 tu, Reli na Sigara zikishuka daraja.

**2. ABDALLAH JUMA- MTIBWA SUGAR (MABAO 25)**

Almanusura straika Abdallah Juma aifikie rekodi hiyo mwaka 2005, alipopachika mabao 25, likiwa limebaki bao moja tu aikute rekodi ya Mmachinga.

Pamoja na kufunga idadi hiyo ya mabao na kuwa mfungaji bora msimu huo, timu yake ya Mtibwa Sugar iliishia kushika nafasi ya saba kwenye msimamo, Yanga ikitwaa ubingwa, Moro United ya pili na Simba ikawa ya tatu, huku Majimaji na Mji Mpwapwa zikiteremka daraja. Anashika nafasi ya pili kwa mabao mengi.

**3. MEDDIE KAGERE-SIMBA (MABAO 23)**

Anakamata nafasi ya tatu kwa mfungaji wa wakati wote Ligi Kuu Bara kutokana na kupachika mabao 23, akiwa mfungaji bora msimu uliopita wa 2018/19.

Meddie Kagere ambaye ni Mnyarwanda, aliisaidia timu yake ya Simba kutwaa ubingwa kwa pointi 93, ikifuatiwa na Yanga iliyomaliza na pointi 86, timu za Stand United na African Lyon zikishuka daraja.

**4. EMMANUEL OKWI-SIMBA (MABAO 20)**


Mganda Emmanuel Okwi, alichukua Kiatu cha Dhahabu msimu wa 2017/18, akipachika mabao 20 kwa msimu akiingia kwenye orodha ya wafungaji bora waliopachika mabao mengi kwenye historia ya Ligi ya Tanzania akiwa wa nne. Ni msimu ambao aliipa Simba ubingwa kwa pointi 69, Majimaji na Njombe Mji zikishuka daraja.

**5. JOHN BOCCO -AZAM FC (MABAO 19)**

Straika ambaye kwa sasa anaichezea Simba, John Bocco, alikuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu msimu wa 2011/12, akipachika mabao 19, yeye anashika nafasi ya tano kwa wafungaji wenye mabao mengi kwenye historia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati huo akiichezea Azam FC, alifunga idadi hiyo ya mabao, lakini hayakuweza kufua dafu na kuifanya timu yake iwe bingwa, kwani iliishia kumaliza na pointi 56, Simba ikiwa bingwa kwa pointi sita zaidi, ikiwa nazo 62, huku timu za Villa Squad, Moro United na Polisi Dodoma zikishuka daraja.

**JE, WAJUA?**




MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi, ana hatua mbili tu zimebakia kuwa kwenye orodha ya mfungaji bora wa wakati wote. Amefunga jumla ya mabao 724 kwa jina lake hadi sasa, ikiwa ni 19 pungufu kwa aliyofunga Cristiano Ronaldo, lakini Muargentina huyo amecheza mechi 100 pungufu kuliko mpinzani wake huyo raia wa Ureno.

www.binzubeiry.co.tz





# Mavunde ataka wenye uhitaji kusaidiwa

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Athony Mavunde, ameziomba taasisi za dini, mashirika ya umma na watu binafsi kusaidia watu wenye uhitaji maalumu kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa corona.

Aidha, kutokana na mlipuko wa virusi vya corona nchini, amewaomba wadau mbalimbali kuwasaidia waumini wasiojiweza wa dini ya kiislamu kuwa kuwapatia misaada ya vyakula vitakavyowawezesha kutimiza moja ya nguzo ya dini hiyo.

Mavunde ambaye pia ni Mbunge wa Dodoma Mjini, alitoa wito huo baada ya kupokea misaada ya chakula wenye thamani ya Sh. milioni 21 uliotolewa na taasisi ya Dar-Ul-Muslimeen kwa kushirikiana na W.I.P.A.H.S kwa waumini wa Msikiti wa Hudda Chamwino jijini Dodoma.

Mavunde alisema kuwa katika kipindi hiki cha janga la ugonjwa wa corona, kuna makundi mengi yanahitaji kusaidiwa mahitaji maalum ikiwamo vifaa vya kujikinga na gonjwa hili.

Aidha, alisema ni wakati pia wa kusaidia misaada ya vyakula kwa waumini wa dini ya kiislamu wanapoendelea mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ili waweze kumudu kutimiza moja wapo ya nguzo ya Waislamu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Dar-Ul-Muslimeen, Shekhe Muslim Bhanji, alisema jumla ya mifuko 300 ikiwamo mchele, maharange, sukari imetolewa kwa ajili ya kuwasaidia waumini wenye uhitaji maalumu wa Msikiti wa Hudda wa Chamwino.

Shekhe huyo alitaja msaada mwingine ni wa sabuni ambapo kwa ujumla vyote vimetolewa ili waweze kujikimu kwenye mfungo wa Ramadhani na pia utasaidia waumini hao kutotembea ovyo kwenye kipindi hiki cha ugonjwa wa corona.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Chamwino, Jumanne Gende, aliwataka waumini waliokabidhiwa misaada hiyo kuitumia kwa malengo yaliyokusudiwa kutoka kwa wahisani hao.

Juma Kemo, Shekhe wa Msikiti wa Hudda Chamwino, akishukuru kwa kupatiwa msaada huo, na kwa niaba ya walengwa aliwataka kuuthamini huku pia wakijilinda na janga la maambukizi ya virusi vya corona kwa kufuata maelekezo ya waatalamu wa afya na viongozi wa serikali.

Kemo alisema jumla ya kaya 80 watasaidiwa misaada hiyo iliyotolewa na wahisani hao, ambao wamedhamiria kusaidia watu wasiojiweza kiuchumi, ikiwamo kwenye kipindi hiki cha janga la maambukizi ya virusi vya corona na kwenye mfungo wa Ramadhani.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi (mbele), akikagua eneo lenye mgogoro wa ardhi Mtaa wa Tambukareli jijini Dodoma mwishoni mwa wiki, alipokwenda kusuluhisha kati ya mimliki wa eneo na uongozi wa Jiji la Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCM yaomba wanaodai kutibu corona kusakwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuwasaka waganga wa kienyeji, ambao wamekuwa wakiwatumainisha watu kuwa wanauwezo wa kutibu ugonjwa wa corona.

Ombi hilo limetolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Dodoma, Dk. Damas Mkassa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini Dodoma.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa mlipuko wa virusi vya corona umezua baadhi ya waganga wa kienyeji, ambao wanadai kuwa wana uwezo wa kutibu janga hilo. Alisema ugonjwa huo jawabu lake ni kupima kwenye hospitali badala ya waganga wa kienyeji, ambao wanadanganya na kuwatapeli watu.

Alisema ugonjwa huo unapimwa kwa kipimo maalum ambacho kinauwezo wa kujua hali ya joto na kubainisha kuwa mhusika ana virusi vya ugonjwa huo ama la.

Dk. Mkassa ambaye pia ni Askofu Mkuu wa Kanisa la Agizo Kuu Tanzania, amewataka kuacha tabia hiyo kwa kuwa watafanya ugonjwa huo kuzidi kusambaa badala ya kuuondoa.

Aliwataka watu kutoufananisha ugonjwa huo na imani ya kishirikina ambao umepitwa na wakati, kwa kuwa vipimo halali vinapatikana hospitalini.

Mwenyekiti huyo amewataka Watanzania kuhakikisha wanatumia vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo vilivyo na viwango vinavyokubalika.

Dk. Mkassa pia ameiomba serikali kuwachukulia hatua kali wanaopotosha jamii kwa kutoa taarifa za uongo kuhusiana na ugonjwa wa corona.

# KKKT yasaidia vifaa vya corona

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA.

JAMII imeombwa kujitokeza kusaidia wafungwa na mahabusi katika kujikinga na ugonjwa homa ya mapafu unayosababishwa na virusi vya corona.

Ombi hilo limetolewa na Mchungaji Evance Mwaunga wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Dodoma Mjini, alipokuwa akikabidhi msaada wa vifaa vya kusaidia kujikinga na maambukizi ya ungnjwa huko kwa viongozi wa Jeshi la Magereza Mkoa wa Dodoma.

Mchungaji Mwaunga, aliomba jamii kuendelea kujitokeza kusaidia Serikali kupitia jeshi hilo katika kuwahudumia wafungwa na mahabusi walioopo kwenye magereza mbalimbali ili kupambana na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema Kanisa hilo liliona litoe msaada huo wa vifaa hivyo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni moja kwa ajili ya kuisaidia Serikali kupambana na maambukizo ya ugonjwa wa homa ya corona.

Alivitaja vifaa hivyo walivyokabidhi kuwa ni barakoa, sabuni za maji na vipande, madumu ya maji 100 pamoja na vitakasa mikono (sanitizer).

Aliongeza kuwa, wamenunua koki za maji kwa madumu yote waliyokabidhi, hivyo jukumu la kuunganisha na sehemu ya kutumika litakuwa la jeshi hilo.

Aidha, alibainisha kuwa vifaa hivyo ni michango iliyotolewa na baadhi ya waumini wa kanisa hilo kwa lengo la kuwasadia wafungwa na mahabusi katika Gereza Kuu la Isanga na Msalato yaliyopo jijini hapa.

Hata hivyo, alisema msaada huo sio mwisho, wataendelea kukusanya vitu na fedha kwa ajili kuendelea kuzisaidia taasisi zingine za Serikali.

Kwa upande wake, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Keneth Mwambinje, akizungumza baada ya kupokea msaada huo, alilishukuru Kanisa hilo kwa kuona umuhimu wa kuwalisaidia wafungwa .

Mwambije alisema msaada huo utapelekwa kwenye maeneo yaliyoelekezwa na wahusika kwa sababu ni kweli yana changamoto ya uhitaji wa vifaa hivyo.

Pia, alisema msaada huo utatumika kwenye magereza hayo mawili na kwenye baadhi ya ofisi za askari wa jeshi hilo kwa ajili ya kujikinga na virusi vya corona.

Aliziomba taasisi na watu binafsi kuendelea kujitokeza kusaidia jeshi hilo kwa sababu kuna uhitaji wa vifaa vingine kwa wafungwa wengine waliopo kwenye magereza ya wilaya za mkoani hapa.





## Wakulima kupewa teknolojia ya kisasa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MTAFITI wa Idara ya Uhifadhi wa Mazao na Usindikaji, kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Tari, Kituo cha Uyole kilichopo mkoani Mbeya, Dk. Andrew Urio, amewaahidi wakulima kusambaza teknolojia sahihi za uvunaji mazao ili kupunguza upotevu wa mazao wakati wa kuvuna.

Dk. Urio aliyasema hayo juzi, alipokuwa akizungumza na Nipashe juu ya mikakati waliyoiweka Tari katika kuwakwamua wakulima na tatizo la upotevu wa mazao shambani.

Alisema walianza kusambaza teknolojia ya uvunaji wa mazao shambani kwa baadhi ya wakulima pamoja na kutoa elimu ya usindikaji kwa lengo la kutunza kinachopatikana.

"Katika kutekeleza mkakati wa taifa wa kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, tunawahamasisha wakulima kutumia teknolojia zetu sambamba na hilo pia tuliwahamasisha wajikite zaidi kwenye usindikaji wa mazao mbalimbali ili kuyaongezea thamani na kujiongezea kipato," alisema Dk. Urio.

Aliongeza kuwa, Idara ya uhifadhi wa mazao na usindikaji ilitoa elimu ya usindikaji kwa baadhi ya mazao kama vile, soya, maharage na viazi lishe ili kutengeneza bidhaa mbalimbali, mikate, keki, bagia, maandazi, juisi na biskuti. Alieleza umuhimu wa elimu wa kuhifadhi mazao kuwa itamuongezea mkulima uhakika wa chakula katika kaya na kuongeza thamani ya soko la bidhaa.

Hata hivyo, Dk. Urio alisema kuwa wanaendelea na mapambano dhidi ya lishe duni kwa kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi namna bora ya kuandaa chakula kitakachokuwa na virutubisho vyote muhimu ili kujenga afya.

Baadhi ya wakulima kutoka Kata ya Tembela iliyopo wilayani Mbeya, waliomba Tari- Uyole kusambaza teknolojia za uvunaji mazao kwa wakulima wote pamoja na kupunguza gharama za uuzaji.

Miongoni mwa wakulima hao, Absolom Mwandafwa, alidai teknolojia hizo huenda zikawa mkombozi kwa wakulima katika kukabiliana na tatizo la upotevu wa mazao shambani, lakini shida iliyopo hazipatikani kwa urahisi na ni ghali.

# Mwakyembe aahidi vifaa vya corona jimboni

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

JUMLA ya vifaa 600 ambavyo ni ndoo 300 na vitakasa mikono 300 vimeahidiwa kutolewa na Mbunge wa Kyela , Dk. Harrison Mwakyembe ambaye pia ni Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ili kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid -19.

Hayo yalithibitishwa jana na Katibu wa Mbunge, Aman Mwakipesile, alipozungumza na Nipashe namna walivyojipanga kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kyela dhidi ya mapambano ya ugonjwa huo hatari.

Mwakipesile alisema vifaa hivyo vitatolewa maeneo yote yanayotoa huduma za kijamii ikiwamo, vituo vya Polisi, mahakama, zahanati, soko stendi za magari na nyumba za ibada.

"Muda wowote kuanzia sasa vifaa hivyo vitawasili wilayani kyela ili kuwasaidia wananchi na tumelenga kuyafikia makundi mbalimbali na maeneo yote ya kutolea huduma lengo ni kuhakikisha watu wananawa mikono kwenye kila sehemu wanayokwenda kupata huduma," alisema Mwakipesile.

Alisema mbali na kusaidia ndoo za maji na vitakasa mikono, pia Mwakyembe yuko kwenye mchakato wa kuwasailiana na wadau mbalimbali ili kusaidia kununua barakoa ambazo zitagawiwa kwa watoa huduma za afya.

Alisema Mbunge alifanya mawasiliano na watu mbalimbali na wameonyesha muitikio, hivyo anasubiria kukabidhiwa barakoa hizo ili zikawasaidie wahudumu wa afya.

Sambamba na hilo, Mwakipesile aliwahamasisha na wadau wengine wenye mapenzi mema na wilaya hiyo kujitokeza kwa wingi kusaidia vifaa kinga kwa ajili ya ugonjwa wa Covid-19.

Mzeenani Said ambaye ni mkazi wa Kitongoji cha Mikumi, Kata ya Bondeni, alisema kipindi hiki cha janga la corona wanahitaji sana faraja hata ya maneno kutoka kwa mbunge wao.




Waendesha bodaboda saba wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ambao jana, walikabidhiwa mkopo wa pikipiki pamoja na tisheti wenye thamani ya Sh. milioni 24 na Taasisi ya Tulia Trust inayosimamiwa na Naibu Spika wa Bunge, Tulia Ackson kwa lengo la kuwasaidia kujikwamua na umasikini. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wenye ulemavu waiomba serikali uboreshaji daftari

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATU wenye ulemavu mkoani Mbeya, wameiomba Serikali kuendelea kuboresha na kutengeneza vifaa rafiki ambavyo vitatumika kwenye uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura awamu ya pili linalotarajiwa kuanza mkoani hapa mapema mwezi ijao.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu Yanzania (Shiviwata), Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Damas Mwambeje, na kusema wanatamani kuona vifaa ambavyo ni rafiki kwao wakati wa zoezi la kuhakiki taarifa zao kwenye daftari la kudumu la wapigakura. Mwambeje alieleza baadhi ya vikwazo wanavyokabiliana navyo wakati wa zoezi hilo ni miundombinu iliyopo kwenye maeneo ya vituo vya kujiandikishia na kuhakiki kwao sio rafiki lakini pia vifaa vinavyotumika vinawapa tabu.

"Tunaomba serikali itusaidie kuangalia upya suala la uboreshaji wa miundombinu ikiwamo majengo, njia za kupitia na vifaa vya kujiandikisha na kuhakiki taarifa kwenye daftari la kudumu la wapigakura ambalo liko mbele yetu hii itasaidia tutimize haki yetu ya kikatiba," alisema Mwambeje.

Katibu wa Chama cha Watu wenye Ulemavu jijini humo, Mawazo Omary ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Disability Green Zone kilichopo Uyole, alisema miongoni mwa vikwazo alivyopata awamu ya kwanza ya kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura ni kushindwa kutia saini la kidole gumba kutokana na vifaa kutokuwa rafiki kwake.

Omary ambaye ni mlemavu wa viungo, alisema alipata shida wakati akijaribu kutia saini kwa kidole gumba hadi alipopatiwa usaidizi na waandikishaji, na kuwa walimbeba.

Aidha, aliishauri Halmashauri ya Jiji la Mbeya kutoa taarifa mapema kwa kundi la watu wenye ulemavu kuwa ni wapi zoezi hilo litafanyika katika kila kata na mitaa kwa madai kuwa itawasaidia kujiandaa mapema ili kushiriki kikamilifu zoezi hilo.

Nipashe ilifanya jitihada za kumtafuta Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, ili kueleza wananchi ni vituo vingapi vitatumika pamoja na vifaa, lakini ziligonga mwamba kutokana na mawasiliano yake kutopatikana.



# RC aonya wasiotii maagizo ya watalaam afya

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, amesema licha ya viongozi na wataalamu wa afya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ya kujikinga na virusi vya Corona bado baadhi ya maeneo kuna changamoto ya kutotii maagizo yanayotolewa hali inayotishia usalama hasa katika mikusanyiko ya watu.

Kufuatia mkusanyiko mkubwa wa watu katika maeneo ya soko la Unguja Ukuu, Serikali ya Wilaya ya Kati kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya hiyo, zimelazimika kuweka utaratibu maalum kwa kila mwananchi anayefika katika minada yote iliyoko katika wilaya hiyo kuvaa barakoa na kufuata taratibu zote zilizowekwa ikiwamo kuacha nafasi angalau mita moja baina ya mtu na mtu.

Vile vile, Hamida alisesema utaratibu uliowekwa si kwa ajili ya masoko ya samaki pekee bali utatumika hata kwa masoko ya kawaida yaliyopo ndani ya wilaya hiyo. Alisema upande wa wafanyabiashara wa maduka wanatakiwa kuepuka kuruhusu mkusanyiko isiyokuwa ya lazima katika maduka yao na ikibainika mbele ya duka la mfanyabiashara kuna mikusanyiko isiyo ya lazima, serikali ya wilaya haitasita kuchukua hatua ikiwamo ya kupokonywa leseni yake ya biashara.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara wa maduka wana tabia ya kuweka maskani katika maduka yao, utakuta mikusanyiko mingi hata kipindi hiki ambacho serikali imekataza na utakuta hiyo mikusanyiko haihitaji huduma yoyote ni mazoea kwa sasa hivi hii hali haitakiwa," alisema.

Naye Ofisa Uhamasishaji kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Mwinyi Issa Khamis, ameipongeza Serikali ya Mkoa wa Kusini kwa juhudi wanazochukua na kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kufanyika mikakati kama hiyo katika mikoa mingine ili kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona.

Nao wananchi waliofika katika maeneo hayo ya soko la Unguja Ukuu wameridhishwa na utaratibu mpya uliowekwa katika eneo hilo la soko ikiwamo uvaaji wa barakoa wakati wanapoenda maeneo ya soko na hata kwenye mkusanyiko wa watu ili kupunguza maambukizo.



Askofu Shao akibariki Sanamu ya Bikira Maria baada ya kuizindua jana, ili kuanza sherehe za kitaifa za miaka 24 tangu kuanzishwa Radio Maria nchini. Sanamu hiyo baadae itapelekwa Jimbo Kuu la Songea ambako itawekwa rasmi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wachimba mchanga kupima joto kabla uchimbaji

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B, Rajab Ali Rajab, amewataka watumiaji wa machimbo ya shimo la mchanga lililopo Kiomba Mvua kupima joto la mwili kabla ya kuingia ili kujiepusha na maambukizo.

Akizungumza na madereva wa magari ya mchanga, wapakiaji na wasimamizi wa shimo hilo, Mkuu huyo wa wilaya alisema, kupima joto, kunawa mikono mara kwa mara, kuvaa gloves na barakoa ndio njia pekee itakayosaidia kupunguza maambukizo ya ugonjwa huo katika shughuli zao za kila siku ambazo zina mwingiliano wa watu.

Alisema serikali ya wilaya imepeleka wataalamu wa afya katika shimo hilo ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo ambao hadi sasa idadi ya maambukizo imekuwa ikiongezeka kila siku visiwani Zanzibar.

Vile vile, alisema hali ya ugonjwa huo katika wilaya yake sio nzuri kutokana na baadhi ya wananchi kukaidi agizo la serikali kuhusu katazo la mikusanyiko kwa kuhudhuria shughuli za mazishi pamoja na kushindwa kutekeleza maagizo ya wataalamu wa afya.

Alisema kuwa serikali haikatazi wananchi kuzika wapendwa wao, lakini ni vyema kwa sasa shughuli za mazishi zikatekelezwa na ndugu wa karibu na marehemu ili kuinusuru wilaya na taifa kwa ujumla dhidi ya Covid -19.

Mkuu huyo pia aliwataka wasimamizi wa shimo hilo kuzingatia makubaliano kwa kuingiza watu 200 kwa siku badala ya 600 wa awali ili kuendelea kujikinga.

Kwa upande wao wapakiaji wa mchanga wamempongeza mkuu huyo wa wilaya kwa kuwapelekea wataalamu wa afya na kuwa wanafanya shughuli zao kwa usalama wa afya zao na familia zao kwa ujumla

Wameahidi pia kutekeleza agizo la serikali kwa kuhakikisha wanaenda katika shughuli zao kwa kuzingatia makundi waliyopangwa.

# Wanaoishi mazingira hatarishi wapewa msaada futari

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR.

ZAIDI ya wananchi 600 wanaoishi katika mazingira magumu katika Shehia za Mbaleni, Kilombero na Kwagube, Mkoa wa Kusini Unguja, wamepatiwa msaada wa vyakula kwa ajili ya kujikimu katika kipindi cha mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akikabidhi vyakula hivyo, Diwani wa Wadi ya Mbaleni, Hassan Ameir, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuhakikisha kila mtu anapata futari ili kutekeleza vizuri ibada ya funga ndani ya mwezi huo.

Alisema katika mwezi huo wa kuchuma, kila mwananchi mwenye uwezo wa kipato ni vyema akawasaidia watu wanaoshi katika mazingira magumu ili nao waweze kujisikia kama wengine katika swala la iftari.

"Katika dunia Mungu ametuumba vipato vyetu vinatofautiana, hivyo kwa wale ambao Mwenyezi Mungu kawapa kipato basi tunawaombea wawe na moyo wa kujitolea zaidi kwa kuwasaidia ndugu zetu ambao kipato chao hakitoshelezi kujikimu mahitaji yao hata ya siku moja," alisema.

Diwani Hassan alisema ni vyema wananchi kutosahau maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya katika kipindi hiki cha Ramadhani kwa kuchukua tahadhari na kuhakikisha kila mmoja anaftari nyumbani kwake ili kujiepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Aliwaomba wananchi hao kuutumia mwezi huo kwa kufanya Ibada kwa wingi na kumuomba Mwenyezi Mungu aondoshe maradhi haya ya Corona ambayo yanatikisa dunia kwa sasa.

Nao baadhi ya wananchi waliopata msaada huo wameshukuru kupatiwa vyakula hivyo hususani katika kipindi hiki kigumu kutokana shughuli zao nyingi kusitasita kutokana ugonjwa huo.

Vyakula hivyo viliyotolewa ni pamoja na mafuta ya kupikia, mchele, sukari, unga wa ngano na tomato.

# Mahakama Kuu yatupilia mbali maombi kuvuliwa ubunge Lissu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetupilia mbali maombi ya kupinga uamuzi wa kuvuliwa ubunge dhidi ya Mbunge wa zamani wa Jimbo la Singida Mashariki, Tundu Lissu.

Katika maombi hayo yaliyosajiliwa kwa namba 42/2019 ya kutaka ridhaa ya Mahakama Kuu kumruhusu kukata rufani yaliyofunguliwa Oktoba 10, 2019, Lissu alikusudia kupinga uamuzi wa kuondolewa ubunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Kudumu za Bunge kutokana na kushindwa kuhudhuria vikao zaidi ya vitatu vya Bunge pasipo ruhusa ya maandishi ya Spika.

Mapema Septemba 9, 2019 mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Sirilius Matupa ulikubali pingamizi la awali la mawakili wa serikali na kutupilia mbali ombi la kuzuia kuapishwa Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Miraji Mtaturu.

Hata hivyo, Lissu aliwasilisha maombi akitaka kuruhusiwa kukata rufani dhidi ya uamuzi wa Jaji Matupa.

Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, walipinga maombi hayo kwa sababu hayakustaili kusikilizwa kwa kuwa yalikinzana na kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Rufani iliyofanyiwa matekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria namba 25 ya 2002.

Upande wa Jamhuri ulidai mahakamani hapo kuwa Lissu hakuwa na haki kisheria kupinga uamuzi wa Mhe. Jaji Matupa wa kumnyima ridhaa kufungua shauri la mapitio ya kiutawala uamuzi ambao uliishia kwa yeye kupoteza ubunge.

Upande wa Jamhuri ulidai, uamuzi wa Jaji Matupa haukupaswa kupingwa kwa njia ya rufani kwa kuwa haukumaliza kesi kama inavyopaswa kuwa kisheria.

Upande wa Jamhuri uliishawishi mahakama kuwa katika kesi mbalimbali, iliamua kuwa rufani haiwezi kukatwa kwa shauri ambalo limeisha katika hatua za awali kama ilivyokuwa kwa kesi ya Lissu ambaye alikuwa akiomba ridhaa ya kuwasilisha maombi ya mapitio na akanyimwa kwa kuwa maombi yake hayakuzingatia sheria.

Aprili 21, mwaka huu mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Yose Joseph Mlyambina, aliyekuwa anasikiliza shauri hilo alitoa uamuzi na kukubaliana na uzito wa hoja za Mawakili wa Serikali na kutupilia mbali maombi ya Lissu ya kutaka ridhaa ya Mahakama Kuu kukata rufani kwenda Mahakama ya Rufani.

Mahakama Kuu iliona kuwa maombi hayo hayana msingi kisheria kwa kuwa sheria hairuhusu rufani kwa kesi inayofafana na hiyo.

Mahakama ilitupilia mbali kesi hiyo na kumtaka Lissu kulipa gharama za kesi hiyo kwa upande wa Jamhuri.

Septemba 9, 2019 Jaji Matupa katika uamuzi wake alisema amesoma maombi ya Lissu, hayatekelezeki kwa sababu mleta maombi alitakiwa kufungua kesi ya kupinga uchaguzi mahakamani, badala yake ameleta maombi ya kutaka kupinga uamuzi wa Spika.

"Mahakama imepata wakati mgumu sana katika kupitia maombi haya," alisema Jaji Matupa na kuongeza kuwa, kama maombi ya Lissu yakikubaliwa yatasababisha uvunjaji wa Katiba kwa kuwa italazimika kuwa na wabunge wawili kwenye jimbo moja na kwamba pia maombi hayo yemechelewa kufikishwa mahakamani.

Hata hivyo Lissu, ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Chadema alisema, alichoomba katika kesi yake ilikuwa ni kutaka Mahakama Kuu itamke kama uamuzi wa kutenguliwa ubunge wake uliochukuliwa na Spika wa Bunge Job Ndugai ulikuwa sahihi kisheria au la, na si kutaka kuipinga Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuitisha uchaguzi au kumpinga, Miraji Mtaturu aliyetangazwa na tume hiyo mshindi wa ubunge wa jimbo la Singida Mashariki.



## HABARI KITAIFA

# Muhimbili yafunga mashine za mil. 210/- za kusafisha damu

**Na Gwamaka Alipipi**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imefunga mashine tatu za kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo, zenye thamani ya Sh. milioni 210.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Umma MNH, Aminiel Aligaesha, ilieleza kuwa hospitali hiyo pia inatarajia kufunga mashine moja ya kusaidia mgonjwa kupumua (ventilator) yenye thamani ya Sh. milioni 56 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana ili kuhudumia wagonjwa waliopata maambukizi ya virusi vya corona.

"Tayari wagonjwa wanaohitaji huduma ya kusafishwa damu wameanza kuhudumiwa na wafanyakazi wa MNH waliopo Hospitali ya Amana tangu Ijumaa majira ya saa 12 asubuhi, ambapo dawa na vitendanishi vya kutoa huduma ya kusafisha figo kwa sasa vinagharimiwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisema Aligaesha.

Alisema sambamba na hilo, MNH imefunga mtambo wa kuchuja maji (Portable RO) wenye thamani ya Sh. milioni 28, mtandao wenye miundombinu ya kusafirisha maji ili kuwezesha mashine hizo kufanya kazi ya kusafisha damu uliogharimu Sh. milioni 12.

"Kutokana na hilo, MNH itapokea madaktari na wauguzi kutoka Hospitali ya Rufani ya Amana kuanzia 28 Aprili, ili kujengewa uwezo kwenye Kitengo cha kusafisha damu pamoja na vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICUs) aina tano tofauti," alisema Aligaesha.

Alisema MNH kupitia Hospitali ya Upanga na Mloganzila, ilipokea wagonjwa 93 kutoka Amana wakiwamo watoto wachanga 30 chini ya mwezi mmoja wakiwa na mama zao, watoto wanne chini ya miaka mitano, kina mama wajawazito 36, wagonjwa wa upasuaji 10 na wagonjwa 13 wenye magonjwa ya ndani.

Alisema MNH imekua bega kwa bega na uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwenye maandalizi ya kupokea wagonjwa waliopata maambukizi ya corona katika Hospitali Rufani ya Amana ikiwa ni hatua ya kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha wagonjwa waliolazwa wanapata huduma.


## VACANCY
### (For reputed Developer)

**Project manager : Posts: 2**
**Qualification :** Civil or Mechanical Engineer, Electrical Engineer 7 years experience in project or site management and should have very high communication skills. Also reference should be from 3 reputed people in the construction industry

**Electrical engineer : Posts: 5**
**Qualification:** Graduation in Electrical
7 years experience

**Electrical technician : Post : 5**
**Qualification:** Diploma in Electrical
5 years Experience

**Plumber : Post :5**
**Qualification:**Diploma in Plumbing
10 years Experience

**AC Technician : Post :3**
**Qualification:** Highly qualified Diploma in Air condition technology
5 years Experience

Very fluent in English and Swahili for all above posts.

***Only Tanzanian citizens for all posts***

***Deadline: 7th May 2020***

**Resumes should be sent to Email : Safari@sura-tz.com & vasudha0606@yahoo.com**





Meneja Mwandamizi wa Masoko Benki ya CRDB, Joe Bendera (wa pili kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Msanii Harmonize (katikati) wakati wa uzinduzi na kampeni ya "POPOTE INATIKI", inayolenga kuwahamasisha wateja kutumia mifumo ya kidijitali kufanya miamala yao ya kifedha. Uzinduzi huo ulienda sambamba na kumtambulisha msanii Harmonize kama balozi mpya wa Benki ya CRDB. Wengine pichani ni wafanyakazi wa Benki ya CRDB na uongozi wa msanii Harmonize. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawatoa hofu wanafunzi mitihani

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imewatoa hofu wanafunzi wenye mitihani ya taifa ambao wako nyumbani kutokana na tishio la corona, kuwa watapata muda wa kutosha kujiandaa kabla ya kuingia kwenye mitihani hiyo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akijibu hoja za wabunge za majadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2020/21.

Alisema kuna taarifa zinasambazwa ambazo siyo za kweli kuwa wanafunzi wenye madarasa na vidato vyenye mitihani watafanya mitihani hiyo shule zitakapofunguliwa, jambo ambalo siyo kweli.

"Tunafanyia kazi mpango ambao utawezesha wanafunzi kusoma na kujifunza vyema kabla ya kufanya mitihani ya kitaifa, wanafunzi wasiwe na wasiwasi kabisa,"alisema na kuongeza:

"Tunafanya tathmini pia kujua ni kwa kiasi gani corona imeathiri uchumi na hasa kwenye sekta ya elimu, tutachukua hatua stahiki na kila kitu kitakaa sawa," alisisitiza.

Alisema, baada ya janga hilo kumalizika serikali itafanya utaratibu wa wanafunzi kumaliza mitaala kama ilivyopangwa na hakutakuwa na mitihani baada tu ya kufungua shule.

Kwa mujibu wa waziri, baada ya shule kufungwa serikali iliondoa ada na tozo mbalimbali kwenye maktaba zake ikiwamo wanafunzi kupata machapisho na majarida kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) baada ya shule kufungwa Mach 17, mwaka huu.

Alisema kabla ya mabadiliko hayo wanafunzi walilazimika kulipa gharama ili kupata machapisho mbalimbali, na kwamba wengi walikwama kwenye suala la usafiri.

"Lakini haitoshi maeneo yenye changamoto tuliandaa vipindi kwa ajili ya televisheni na Aprili 20, mwaka huu vilizinduliwa kwa kushirikiana na televisheni mbalimbali zikiwamo redio zaidi ya 34."

"Wakifungua shule hakuna cha mitihani wala majaribio, hivyo elekezeni akili kwenye kujikinga msiwe na wasiwasi wawote mkiwa nyumbani," alisisitiza Prof. Ndalichako.

Alivionya vyuo na shule ambazo zimeanza kutoa matangazo ya kuwataka wanafunzi kurudi shuleni, na kwamba watakaobainika kufanya hivyo watachukuliwa hatua kali kwa kuwa shule zitafunguliwa kwa tangazo la Waziri Mkuu.

Awali, Waziri Kivuli wa Elimu, Suzan Lyimo, alisema kuna zaidi ya wanafunzi milioni 14 kati yake 12,043,577 wa msingi na 2,023,457 sekondari wako nyumbani tangu serikali itangaze kufunga shule.

Aliitaka serikali kuja na mpango mkakati wa kusaidia elimu kwa njia ya masafa kwa shule za msingi na sekondari na kwamba nchi kama China, Italia, Ufaransa, Ujerumani, Saudi Arabia na Vetinamu zinafanya hivyo.


## MAADHIMISHO YA MIAKA 56 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR



THE H.E. DR. JOHN POMBE MAGUFULI
PRESIDENT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



H.E. ALI MOHAMED SHEIN
PRESIDENT OF THE REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR

Menejimenti na wafanyakazi wa **The Guardian Limited** tunatoa pongezi za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, na Watanzania wote** kwa kuadhimisha miaka **56 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.**

The Guardian Limited

615717602




# COSTA AMTEMEA 'NYONGO' CONTE

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, hangeweza kumaliza msimu wote kama kocha wa Real Madrid, kwa mujibu wa nyota wa Atletico Madrid, Diego Costa.

Conte na Costa walifanya kazi pamoja pale kwa miamba wa Ligi Kuu ya England, Chelsea kabla ya yeye kuondoka Stamford Bridge kwenda Atletico baada ya kushindwa kuelewana na kocha huyo raia wa Italia msimu wa 2016-17.

Alipoulizwa kuhusu Conte, Costa aliambia ESPN Brasil: "Sisi [Conte na mimi] tulikuwa na matatizo nje ya uwanja, lakini nafikiri ni kocha mzuri.

"Sina hisia mbaya na Conte. Lakini kuwa kocha wa daraja la juu, juu zaidi anatakiwa kubadilika kwenye mambo ya utawala. Ni msumbufu. Angekuwa katika timu kama Real Madrid asingeweza kudumu hata kwa msimu mmoja."

Costa alizaliwa nchini Brazil na alicheza mechi mbili kwa ngazi ya vijana kabla ya kuamua kuiwakilisha Hispania mwaka 2013.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amecheza mechi 24 kwa kikosi cha Hispania, pia alikuwapo kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018.



# Barca yawapotezea Neymar na Martinez

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona haifanyi makubaliano yoyote na nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar au mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, kwa mujibu wa Rais wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas.

Miamba hao wa LaLiga kwa muda mrefu wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Neymar na Martinez na wametajwa kwamba wanaweza kuwatwaa kipindi cha majira ya joto kinachokuja. Hata hivyo, Tebas ametupilia mbali madai hayo, akisema Barca wana kipaumbele kingine hasa wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

"Si kweli kwamba kwa sasa wanafanya makubaliano na Barca kuhusu kuwasajili wachezaji hao wawili," alisema akiiambia Adea Conecta Ijumaa. "Kwa sasa wanafikiria zaidi namna gani watakavyorudi msimu huu wa ligi utakapoanza tena. Usajili wa wawili hao unaweza kuufanya kwa siku za usoni, lakini kwa sasa hicho si kipaumbele chao.

"Kwa sasa wanaangalia shughuli inavyoendelea ndani ya klabu. Hakuna Neymar au Lautaro, majina haya si kipaumbele cha Barca kwa sasa."

Tebas aliongeza: "Klabu kwa sasa haina nafasi ya kufanya usajili mkubwa." Msimu wa LaLiga ulisimama mwezi uliopita kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, ambavyo vimeua watu zaidi ya 22,500 nchini Hispania.

# Maddison atangaza kubaki Leicester

**LONDON,** England

NYOTA wa Leicester City, James Maddison, amesema "bilashaka" atabakia katika klabu hiyo licha ya kuhusishwa na mpango wa kuwaniwa na Manchester United.

Kiwango cha Maddison alichokionyesha pale Leicester kimemfanya kuonekana kuwa kwenye rada za kocha, Ole Gunnar Solskjaer kule United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 wa timu ya Taifa ya England, mkataba wake na Leicester unamalizika mwaka 2023.

Alipoulizwa kama atabakia pale Leicester, Maddison alisema kupitia BT Sport: "Bilashaka nitabaki."

Maddison aliongeza: "Ilikuwa moja ya uamuzi wangu bora kabisa niliyowahi kuufaya, kuja hapa. Napapenda."

Leicester ilimsajili Maddison kutoka Norwich City mwaka 2018 kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 20.

Maddison amekuwa na kiwango cha kuvutia pale kwenye Uwanja wa King Power, ambapo amefunga mabao 16 katika mashindano yote tangu atue.



# Haaland akunwa na mashabiki Dortmund

**DORTUMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland amesema kusikia mashabiki wa Borussia Dortmund wakiimba wimbo wao marufu wa 'Yellow Wall' na kulitaja jina lake ulikuwa wakati wa hisia kali zaidi katika maisha yake.

Haaland aliwasili pale Dortmund kutoka Salzburg Januari, akiwa tayari amefunga mabao 28 katika mashindano yote, yakiwamo nane kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alicheza mchezo wake wa kwanza kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati akifunga hat-trick akitokea benchi.

Katika mahojiano na tovuti ya Dortmund, Haaland, ambaye pia alihusishwa sana na kujiunga na Manchester United, alizungumzia mapokezi ya aina yake aliyoyapata kutoka kwa mashabiki pale kwenye Uwanja wa Signal Iduna Park.

"Nikiwa mkweli, huu umekuwa mmoja wa wakati wangu bora kabisa katika maisha yote," alisema Haaland, ambaye alibainisha kwamba anatumia muda wake mwingine kufanya mazoezi ndani kwake wakati huu ambao hawaruhusiwi kutoka ndani.

"Wakati kile kinatokea, kwa hakika ulikuwa wakati wa kuvutia zaidi. Nilihamasika sana.

"Kuona wimbo wa Yellow Wall ukiimbwa na mashabiki na kutaja jina langu, hakika kabisa nilipata hisia za aina yake. Hisia ambazo sijawahi kuwa nazo."







# COUTINHO ANUKIA KUBAKISHWA BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wanaweza kumbakisha Philippe Coutinho kuendelea kukipiga kwenye kikosi hicho, kwa mujibu wa kocha, Quique Setien

Coutinho, ambaye kwa sasa yupo kwa mkopo kule Bayern Munich, kwa muda sasa, amekuwa akihusishwa sana kuondoka moja kwa moja pale Barca.

Kocha wa Barcelona, Setien amebainisha kwamba amepata suluhisho la Coutinho na anaweza kumchezesha nyota huyo wa Brazil nafasi ya kiungo wa kati, kwa mujibu wa gazeti la Marca.

Setien anaona kwamba, Coutinho anaweza kufiti zaidi kama akicheza nafasi ya kiungo wa kati kwenye kikosi chake kuliko kumuuza.

Ripoti hiyo imesema kwamba, Setien anaona Coutinho atafaa zaidi kucheza namba nane na kwamba atakuwa na nafasi.

"Kocha (Quique) Setien bado anaona kuna nafasi kwa Coutinho ndani ya kikosi cha Barcelona, hivyo anaweza kumbakisha Nou Camp," limeandika gazeti la Marca.

Coutinho amecheza mechi 32 kwenye mashindano yote msimu huu pale Bayern Munich na amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda Ligi Kuu ya England.

# *Immobile: Inzaghi ni kama Klopp tu*

**ROME,** Italia

CIRO Immobile amemlinganisha kocha wa Lazio, Simone Inzaghi na kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, wakati nyota huyo wa Italia akibainisha ndoto yake kwa Napoli.

Lazio ya Inzaghi ilikuwa imepitwa pointi moja tu na mabingwa na vinara Juventus baada ya mechi 26 wakati msimu wa Serie A uliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Lazio imeshatwaa ubingwa wa Coppa Italia (2019) na Supercoppa Italiana (2017 na 2019) chini ya Inzaghi, ambaye alichaguliwa mwaka 2016.

Immobile alifanya kazi na Klopp wakati alipokuwa kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, akiwa na Borussia Dortmund msimu wa 2014-15 na mshambuliaji huyo wa Lazio amemsifia Mjerumani huyo kwa kumlinganisha na Inzaghi.

"Klopp ni kocha wa aina yake na mara zote nimesema kwamba ningependa kufanya kazi na yeye wakati ambao nikiwa kwenye kiwango bora. Ni kocha aliyekamilika, ana kila kitu," alisema Immobile kupitia Instagram Live.

Immobile amefunga mabao 27 kwenye Serie A msimu huu wakati ligi hiyo ikisimamishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu, COVID-19.

Huku mechi 12 zikiwa zimesalia ligi hiyo kumalizika, Immobile anakaribia rekodi ya Gonzalo Higuain ya kufunga mabao 36, kwa msimu mmoja wa Serie A, ambayo aliiweka wakati akiwa Napoli msimu wa 2015-16.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID NA NDOTO NDEFU KWA NEYMAR

Wakala asema, bado Rais Florentino Perez anamuota na bei yake ni kama Messi na...

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, kwa muda mrefu ameonyesha nia ya kutaka kumsajili Neymar akacheze pale Santiago Bernabeu, wakala wa zamani wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, Wagner Ribeiro amedai.

Wakala Ribeiro amezungumza katika mahojiano na ESPN kwenye kipindi cha 'Canal do Nicola', ambapo amesema mchezaji huyo wa Paris Saint-Germain na nyota wa zamani wa Barcelona amekuwa akiwaniwa na miamba hao wa mji mkuu wa Hispania kwa miaka mingi.

Kwa mujibu wa Ribeiro, yeye na Perez walizungumza mara kadhaa kuhusu Neymar, pamoja na kukutana mapema mwaka jana.

**Ribeiro amekuwa akihusika na kupeleka wachezaji kadhaa wa Brazil pale Madrid, lakini Neymar amebakiwa kuwa anawaniwa na mabingwa hao mara 13 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.**

Kwa miaka kadhaa, Ribeiro alikuwa mwakilishi wa Neymar mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akiongozwa na baba yake mzazi kwa kipindi cha muongo mmoja.

Ribeiro na Neymar walikuwa pamoja wakati Chelsea walipomfuata mshambuliaji huyo mwaka 2010 wakati huo akiwa pale Santos, na Ribeiro amedai kwamba Bayern Munich na Juventus pia walionyesha nia kubwa ya kutaka kumsajili kabla hajaenda pale Camp Nou.

"Nilikwenda Madrid mara nyingi sana, kwa sababu Florentino alikuwa na ndoto ya kutaka kumsajili Neymar," alisema Ribeiro.

"Mwaka jana, Mei nilikuwa naye kwenye ofisi yake na aliniambia bado ana ndoto ya kumsajili Neymar."

Neymar sasa anaweza kununuliwa kutoka PSG kwa euro milioni 164, kwa mujibu wa Ribeiro, ambaye amesema anamlinganisha na Lionel Messi au Cristiano Ronaldo.

"Ni mchezaji bora kabisa," amesema Ribeiro. "Kamwe sijawahi kumuona Neymar akicheza vibaya. Kila mechi anacheza vizuri."

## ZISIKUPITE

### PSG YAJITOSA KWA POGBA

KLABU ya Paris St-Germain imetoa ofa kwa kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 27, pamoja na nyota wa Argentina, Angel di Maria, 32, ambaye alishindwa kung'ara pale Old Trafford mwaka 2015 - kama sehemu ya mpango huo. ***(Mail on Sunday)***

### KLOPP KWA BABA MBAPPE

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amempigia simu baba mzazi wa Kylian Mbappe kujadiliana naye kuhusu mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anayekipiga pale Paris St-Germain na timu ya Taifa ya Ufaransa kwa ajili ya uhamisho wake. ***(Le10Sport)***

### SPURS YAMTAKA RAKITIC

KLABU ya Tottenham Hotspur, imejiunga kwenye mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Barcelona na Croatia, Ivan Rakitic, mwenye umri wa miaka 32. ***(Mundo Deportivo)***

### DORTMUND KUMSAJILI SAKA

MIAMBA wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Borussia Dortmund, wanaangalia uwezekano wa kumsajili mlinzi wa Arsenal, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 18. ***(Sunday Mirror)***

### PSG KUMZUIA MBAPPE REAL

KLABU ya Pari St-Germain itakuwa tayari "kumuweka benchi Kylian Mbappe" kuliko kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, kwenda Real Madrid. ***(Sun on Sunday)***

### EVERTON KWA KOOPMEINERS

KLABU ya Everton inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 12 kwa ajili ya kumnunua kiungo wa AZ Alkamaar ya Uholanzi, Teun Koopmeiners mwenye umri wa miaka 22, na wanaweza kumuuza mshambuliaji wao Muitaliano, Moise Keane, 20, kwenda Inter Milan. ***(Sun on Sunday)***

### DORTMUND NA SANCHO

KLABU ya Borussia Dortmund inaamini ushawishi wao kwa winga Muingereza, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 20, kubakia klabuni hapo licha ya uvumi kumhusisha na kwenda Manchester United. ***(Teamtalk)***

### MOURINHO AMGEUKIA MEUNIER

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, binafsi amempigia simu mlinzi wa PSG, Mbelgiji Thomas Meunier, mwenye umri wa miaka 28, ili kujaribu kupata saini yake kipindi cha majira ya joto. ***(Sunday Express)***

### BARCA, SPURS VITANI

KLABU ya Barcelona na Manchester City, zinawania kumsajili mlinzi wa Benfica mwenye umri wa miaka 22, raia wa Ureno, Ruben Dias. ***(Record)***

### ARSENAL MGUU KWA PARTEY

KLABU ya Arsenal itahitaji kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao ili kuweza kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey, 26. ***(Sunday Express)***

### CHELSEA KUMPOTEZEA CHILWELL

KLABU ya Chelsea inapanga kuachana na mpango wao wa kuwania kumsajili beki wa pembeni wa Leicester na timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell mwenye umri wamiaka 23. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# Sebo amulika nje ya Afrika

**Na Hawa Abdalla,** ZANZIBAR

MCHEZAJI wa Azam FC, Abdallah Kheri "Sebo" amesema malengo yake makubwa ni kuona siku moja ndoto yake ya kucheza soka la kulipwa nje ya Afrika inatimia.

Beki huyo wa Azam FC, kwa sasa yupo kwao visiwani hapa baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara kusimama kwa kipindi kisichojulikana kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19).

Akizungumza na gazeti hili juzi, Sebo alisema anacheza soka kwa bidii na kulipenda ili kuona ndoto yake ya kucheza soka nje ya Africa inatimia kwani hayo ndio malengo yake makuu tangu anaanza safari kisoka.

Alisema kila mchezaji anatamani siku moja atimize malengo yake, hivyo hata yeye anatamani lengo lake hilo litimie na ndio maana anafanya jitihada pindi anapopangwa ili kuona kiwango alichokuwa nacho kinaimarika zaidi.

"Sasa hivi siangalii tena kucheza ligi ndani ya klabu za Afrika, naangalia zaidi nje ya Afrika na endapo ndoto yangu hii itatimia, basi nitafurahi sana, natumia muda mwingi kufanya mazoezi ili kuhakikisha nakuwa na kiwango kizuri zaidi," alisema.

Aidha, akizungumzia ushindani wa Ligi Kuu Bara, alisema timu za Tanzania Bara zinaushindani wa hali ya juu kutokana na kuwapo kwa wachezaji wazuri wanaosajiliwa kutoka nchi mbalimbali, na kwamba kama mchezaji unatakiwa ujitume ili kocha akupange katika kila mechi.

"Ukiacha ushindani wa ligi, lakini pia timu zenyewe zinaushindani, maana mchezaji unatakiwa uwe na kiwango cha kumshawishi kocha akupange uwanjani katika mchezo, na akupange katika timu ambazo ni ngumu na zimefanya usajili wa wachezaji wengi kutoka nje ya nchi, hilo huongeza ushindani wa wachezaji," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wachezaji wenzake hasa waliopo visiwani Zanzibar kutokata tamaa na kuendeleza vipaji vyao kwa kucheza mpira kwa kuwa soka ni mafanikio ya muda mrefu endapo litatendewa haki.

"Bado baadhi ya wachezaji hapa Zanzibar hawajawa makini katika soka, wanachukulia kama sehemu ya kutafuta kazi na wakishaajiriwa hawajitumi tena kwa kuviendeleza viwango vyao, Mimi binafsi nilikuwa askari lakini niliacha kazi hiyo kwa ajili ya mpira kwakuwa naupenda kutoka moyoni na naamini kama utanipa ridhiki na umaarufu pale tu nitakapofanya vizuri,'alisema.

Alisema tangu aanze kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, anaona kiwango chake kinazidi kuimarika zaidi anavyocheza mechi pamoja na yeye mwenyewe kujituma kwa kufanya mazoezi binafsi.

# KATWILA AJIVUNIA VIPAJI LUKUKI MTIBWA SUGAR

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuber Katwila, amesema klabu hiyo ni chuo cha kuzalisha vipaji na ana imani ya kukiboresha kikosi chake endapo baadhi ya nyota wake watapata nafasi ya kusajiliwa na timu zingine.

**Kauli hiyo imekuja baada ya kuzagaa kwa taarifa kuwa kuna baadhi ya nyota wake akiwamo Salim Kihimbwa na Abdulhalim Humud, kutajwa kutakiwa na Yanga inayowania kuinasa saini yake kwa ajili ya msimu ujao.**

Katwila ameliambia gazeti hili kwamba, hana tatizo wala hofu juu ya nyota wake hao kutakiwa na timu zingine kutokana na kujawa na imani ya kupata mbadala wao kutokana na timu yao kuwa na hazina kubwa ya vijana.

Alisema kuwapo kwa hazina ya nyota wengi katika klabu hiyo kwa upande wa timu ya vijana, kunamfanya ajivunie na kutokuwa na presha ya baadhi ya nyota wake kutajwa kutakiwa na timu nyingine.

"Kwa upande wangu sina hofu na wachezaji hao au wengine kutakiwa kwenda kupata ushindani katika timu zingine, kwa sababu kwetu ni chuo, hivyo kama itatokea wakaondoka, nitapata wachezaji ambao wataziba nafasi zao," alisema Katwila.

Alisema kwa sasa bado wapo kimya juu ya nafasi watakazosajili kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa kuendelea na baadhi ya nyota wake wa kikosi cha kwanza wanaotajwa kutakiwa na timu nyingine.

Ligi Kuu Bara imesimamishwa kwa muda usiojulikana kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona na wachezaji wapo nyumbani wakiendelea kufanya mazoezi binafsi pamoja na kuchukua tahadhari dhidi maambukizo ya virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

## KASEJA HATANII...



Kipa mkongwe nchini, Juma Kaseja, anayeichezea KMC FC ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, akiruka juu kudaka mpira wakati akifanya mazoezi binafsi, kipindi hiki timu zote zikiwa zimesitisha mazoezi ya pamoja na wachezaji wao kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *TFF, TPLB wapewa mbinu kumaliza ligi*

**Na Saada Akida**

HUKU majaliwa ya kurejea kwa Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza yakiwa bado hayajulikani, Makamu Mwenyekiti wa JKT Tanzania, Tabit Baraja, amesema kwa mtazamo wake anaona ni bora Shirikisho la Soka nchini (tff) na Bodi ya Ligi (TPLB) kutafuta vituo viwili ambavyo vitatumika kwa ajili ya ligi hizo mbili kuchezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraja alisema jinsi hali inavyozidi kwa wagonjwa waliopata maambukizi ya virusi vya corona, hataki kuona ligi hiyo ikifutwa na badala yake TFF na TPLB itafute kituo kimoja na ligi hiyo pamoja na ile ya Daraja la Kwanza kuendelea kuchezwa bila mashabiki.

"Bora ligi ichezwe bila mashabiki ili kupatikana bingwa pamoja na msimu ujao kupata idadi ya timu wanazopaswa kupanda, kama vile Ligi Kuu itachezwa Dar es Salaam na kumuomba mdhamini akubali kutoa gharama za timu kwa sehemu ya kufikia na mahitaji muhimu.

Pia Daraja la Kwanza na la Pili watafutiwe kituo chao ili nao waendelee kupatikane timu ambazo zitashiriki Ligi Kuu msimu ujao na zitakazopanda Daraja la Kwanza," alisema Thabit.

Alisema ikichukuliwa uwamuzi wa kuifuta ligi itakuwa harasa kwa timu za Daraja la Kwanza hasa zile ambazo tayari zimejihakikishia kucheza Ligi Kuu pia timu zitazotakiwa kushuka daraja.

# Michezo

Jumatatu Aprili 27, 2020

Nipashe




Madrid na ndoto ndefu kwa Neymar

UKURASA 22

WAMEKUBALI...



Mshambuliaji wa Aston Villa, Mtanzania Mbwana Samatta akishangilia sambamba na kiungo wa timu hiyo, Mzimbabwe Marvelous Nakamba (kushoto) baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikilala 2-1 kwenye fainali ya Kombe la Ligi (EFL Cup) Machi 2, mwaka huu. Wachezaji wote wa Aston Villa wamekubali kukatwa asilimia 25 ya mishahara yao kipindi hiki cha janga la corona. **PICHA: MTANDAO**

## Costa amtemea 'nyongo' Conte

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, hangeweza kumaliza msimu wote kama kocha wa Real Madrid, kwa mujibu...



HABARI UK.20

## Wafungaji wa5 wa wakati wote Bara

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA inaonyesha kuwa, mfumo wa Ligi Tanzania Bara uliozishirikisha timu zote nchini ulianza rasmi mwaka..



HABARI UK. 14

# SAMATTA AFYEKWA MSHAHARA ENGLAND

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Akatwa asilimia 25 kwa miezi minne mfululizo, Aston Villa yatoa sababu kuwa ni...

HUKU akiendelea kujifungia ndani kukwepa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu (COVID-19) kama ilivyo kwa wachezaji wenzake, mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, amekumbana na panga kali kwenye mshahara wake wa kila wiki katika klabu ya Aston Villa, ambapo atakuwa akikatwa asilimia 25 kwa kipindi cha miezi minne, imeelezwa.

Hata hivyo, panga hilo halitatembezwa kwenye mshahara wa Samatta pekee, bali kwa wachezaji wote wa Aston Villa, na benchi la ufundi la kikosi cha kwanza na viongozi wakuu wa klabu hiyo wote wamekubali kukatwa kiasi hicho katika mishahara yao kila wiki kutokana na janga la COVID-19 ili kuisaidia klabu hiyo kusonga mbele, taarifa ya Aston Villa ilieleza juzi, Jumamosi.

**Villa inakuwa klabu ya hivi karibuni kutoka Ligi Kuu England kutangaza uamuzi huo wa wachezaji, baada ya Southampton, West Ham United, Watford na Sheffield United kuchukua hatua kama hiyo.**

Shughuli zote za soka England zilisimama kuanzia mwezi uliopita kutokana na mlipuko wa janga la virusi vya corona.

"Wachezaji wa kikosi cha kwanza, makocha wa kikosi cha kwanza na viongozi wakuu wote wamekubali kupunguzwa kwa mishahara yao kwa asilimia 25 kwa kipindi cha miezi minne kuisaidia klabu katika kipindi hiki cha kutokuwa na uhakika," Ofisa Mtendaji Mkuu wa Villa, Christian Purslow alisema.

Aliongeza kuwa, mapitio zaidi yatafanyika mwishoni mwa kipindi cha miezi minne.

Arsenal ilitangaza makato ya asilimia 12.5 kwa wachezaji wake na viongozi wa benchi la ufundi tangu ligi hiyo iliposimama, wakati Liverpool, Tottenham Hotspur na Bournemouth walibadilisha uamuzi wao wa awali ili kuwachanganya wafanyakazi wasiokuwa wachezaji kutokana na kukosolewa.

Mapema Jumamosi, Norwich City ilitetea uamuzi wake kwa wafanyakazi, wakati Chelsea ilisema wachezaji wao wa kikosi cha kwanza hawatakumbana na panga hilo la mishahara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >